# Nipashe

Jumanne Agosti 23, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581046

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




Nipashe TESA

Jumanne Agosti 23, 2022 TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Msaada kisheria unavyoinua haki za wanyonge na kinamama vijijini Ukurasa 13

Wenye ulemavu hawa wana jambo lao elimu ya kidigitali Ukurasa 12

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBITI

Kilimo kinavyowaathiri mabinti Kibiti, chaweka mazingira ya mimba utotoni

■100 waanguka sekondari, msingi miaka 2

KUNA usemi kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa taifa, kuwa ndicho kinachozalisha chakula kutoka kwenye mazao na mifugo tena ni chanzo cha malighafi za viwanda vingi.

Lakini, wapo baadhi wanaoweza kukilaani kuwa kimekuwa chanzo cha kubadilika na kuharibika maisha yao, hawa ni wasichana kwa sababu wapo waliobakwa wakilinda (kuamia) mazao shambani au wakilisha mifugo porini. Zote ni kazi za kilimo.

Kwa wanafunzi wa Halmashauri ya Kibiti Mkoa wa Pwani, kimekuwa uti wa mgongo wa mimba za wanafunzi na mabinti vijijini, kwa sababu walezi na wazazi wanapokwenda mashambani na kuwaacha watoto peke yao nyumbani 'waharibifu' hutumia mwanya huo kuwaghilibu na kuwaacha wajawazito.

Inaelezwa kuwa wakulima hao hukaa mashambani na kurejea baada ya miezi sita na hapo wasichana wengi wanadanganywa na kupewa mimba na kuacha shule.

Wasichana wana haki ya kulindwa ili wasome na kumudu maisha yao. PICHA: MTANDAO

UKURASA 11

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa


BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT 1,025,118,259 KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Mtoto** wa Mrema aanika wosia wa baba yao, tarehe ya maziko yatajwa

UKURASA 2



# Samia: Ni sensa bora zaidi Afrika

• **Yazingatia** mikakati ya kitaifa, kikanda na kimataifa, aonya... *Endelea ukurasa 2*




## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**MTOTO WA SIMBACHAWENE KIZIMBANI KESHO**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema linatarajia kumfikisha mahakamani kesho mtoto wa...

UKURASA WA 19

**ODINGA ATINGA KORTINI KUPINGA MATOKEO YA UCHAGUZI**

MGOMBEA wa urais wa Chama cha Muungano wa Azimio, Raila Odinga, amewasilisha rasmi ombi la kupinga...


## Mwinyi: Mrema alikuwa tishio CCM

UKURASA 4



## Shangazi aua mtoto akidhani ni ng'ombe

UKURASA 2


MICHEZO **SIMBA KUIVAA ASANTE KOTOKO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia: Ni sensa bora zaidi Afrika

**Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema sensa ya watu na makazi ya sita inayofanyika leo nchini, ni ya kipekee barani Afrika na muhimu kutokana na kuzingatia mikakati iliyopo kitaifa, kikanda na kimataifa.

Amesema upekee wa sensa hii umetokana na kuunganishwa na sensa ya majengo yote nchini kwa lengo la kufahamu kiwango cha ubora wa makazi ya wananchi wanayoishi, jambo ambalo halijawahi kufanyika.

Akiwahutubia Watanzania usiku wa kuamkia siku ya sensa kupitia vyombo vya habari, Rais Samia alisema mbali na kusaidia kupata taarifa kamili na za uhakika zitakazoisaidia serikali kuandaa vizuri zaidi mipango ya maendeleo, sensa pia itaifanya Tanzania kuwa nchi pekee Afrika kuunganisha sensa ya watu na makazi.

Alisema baadhi ya majibu ya maswali yatakayoulizwa kwenye sensa, yatapima na kutathmini utekelezaji wa ajenda za kikanda na kimataifa kama vile Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2050, Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya Mwaka 2063 na Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya Dunia ya Mwaka 2030.

"Kukamilika kwa zoezi hili kutaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza katika Bara la Afrika kuunganisha Sensa ya Watu na Makazi," Rais alisisitiza.

Alizipongeza kamati za sensa ngazi ya taifa kwa weledi mkubwa waliouonyesha kufanikisha maandalizi, zikiongozwa na Mwenyekiti wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Mwenyekiti Mwenza, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah.

Mkuu wa Nchi aliwaomba Watanzania kutoa ushirikiano kwa makarani wa sensa ili wafanye kazi yao na kupata takwimu sahihi za watu na makazi zitakazozaa mafanikio makubwa yaliyokusudiwa.

"Niwasisitize wananchi wote kutoa taarifa za watu wote, hata wale wenye ulemavu na kuachana na mila potofu za kuwaficha watu hao, kwani kila Mtanzania ana haki na nafasi yake bila kujali hali yake," alisema.

Aliwaomba viongozi wa dini, kisiasa, kimila na kijamii kuendelea kuwakumbusha wanakaya kutoa taarifa kamili na za uhakika kwa makarani watakaopita kwenye maeneo yao.

Rais Samia aliwahakikishia Watanzania kuwa taarifa zitakazokusanywa na makarani ni siri kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu, Sura 351.

"Karani wa sensa haruhusiwi kutoa siri ya taarifa aliyokusanya katika kaya. Akifanya hivyo kwa makusudi ni kosa la jinai, hivyo hatua za kisheria zitachukua mkondo wake," alisisitiza.

Sensa hufanyika mara moja kila baada ya miaka 10. Zilizokwishafanyika ni miaka ya 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.

Kwa mujibu wa Rais Samia, kabla ya Uhuru, kumbukumbu zinaonyesha Tanzania Bara wakati huo ikitambulika Tanganyika, ilifanya sensa tano ikiwa ni kuanzia mwaka 1913 na nyingine miaka ya 1921, 1931, 1948 na 1957.

Alisema kwa Zanzibar, sensa ilifanywa moja mwaka 1958 wakati wa ukoloni na utawala wa Sultan na kwamba zilikosa vigezo vya kisayansi kwa kuwa zilifanyika kwa malengo mahsusi ya watawala wa wakati huo, kujua idadi ya manamba, idadi ya watu wanaoweza kwenda vitani na malengo mengine ya wakati huo.



Mratibu wa magonjwa yasiopewa kipaumbele (NTDs), kutoka Ofisi ya Shirika la Afya Duniani (WHO), Tanzania, Dk. Alphoncina Nanai, akizungumza katika mkutano wa ushauri wa kitaalamu wa kutokomeza ugonjwa wa usubi, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shangazi aua mtoto akidhani ni ng'ombe

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

MTOTO Braun Kaduma (7), mkazi wa Kijiji cha Kichiwa, Kata ya Kichiwa, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, amefariki dunia kutokana na kipigo kutoka kwa shangazi yake, Estaroda Kaduma aliyekuwa kwenye maombi usiku.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamis Issah, alisema tukio hilo limetokea Agosti 20, mwaka huu, majira ya saa nane usiku nyumbani kwao wakati mtoto huyo akiwa amelala.

Kamanda Issah alisema kuwa kwa mujibu wa mahojiano na shangazi huyo, mtuhumiwa alikuwa anafanya maombi na katika maombi hayo, aliona ng'ombe mweusi mkubwa ametokea na kuanza kumpiga.

"Alisema ameona ng'ombe mkubwa katika eneo lake wakati akifanya maombi ya usiku, akawa anampiga mpaka yule ng'ombe akaondoka. Baadaye anaambiwa 'hukuwa unampiga' ng'ombe, ulikuwa unampiga mtoto mdogo ambaye amefariki dunia'.

"Mtoto amepoteza maisha kwa imani ambazo kwa kweli hata sisi wenyewe Jeshi la Polisi tumeshangaa, huyu mama tumemweka chini ya ulinzi kama mtuhumiwa na sheria itafuata mkondo wake kama tukio lilivyotokea. Hatuwezi kuamini imani nyingine ilhali watoto wadogo kama hawa wawe wanapotea," alisema.

Kamanda Issah alibainisha kuwa mtoto huyo alikuwa analelewa na shangazi yake huyo baada ya baba yake kuugua ugonjwa wa akili.

Alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe linatoa wito kwa wananchi mkoani humo kuwa karibu na kufuatilia mienendo yote dhidi ya watoto.

"Sasa kumekuwa na matukio yanayohusisha watoto wadogo, watoto wanapoteza maisha katika matukio ya kujinyonga au kunywa sumu. Wazazi tusiwe wakatili kiasi kwamba mtoto anahofu na maisha yake, anaona kheri kujitoa uhai kulikoni kukutana na mzazi katika kumpa adhabu.

"Sasa kama tukio hili mtoto hajakosea chochote, eti mzazi unasema alikuwa kwenye maombi, hii haikubaliki," Kamanda Issah alionya.

# Wosia wa Mrema wawekwa hadharani

**Na Waandishi Wetu**

MICHAEL Mrema, mtoto wa Mwenyekiti wa Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), Augustino Mrema, ameeleza walichoteta na baba yake kabla ya umauti kumfika juzi.

Akizungumza nyumbani kwa baba yake jana mkoani Dar es Salaam, Michael alisema kuwa Jumamosi ya Agosti 20 saa 11 jioni walipata nafasi ya kuzungumza na baba yake na miongoni mwa alichowaambia ni kuishi kwa upendo, amani na kupendana katika familia yao.

"Siku ile ya Jumamosi (Agosti 20) tulipozungumza naye akiwa yuko vizuri na anacheka tu, hatukutegemea kama Jumapili asubuhi angetuacha.

"Baada ya kuzungumza naye, tulifanya maombi kumwombea apone haraka na miongoni mwa alichozungumza ni kututaka tuishi kwa amani, kupendana na kuishi salama kama familia," alisema Michael.

Alisema miongoni mwa vitu ambavyo hawatovisahau kwa baba yao ni ucheshi.

"Baba amefanya mambo makubwa ikiwamo kutusomesha na tukapata kazi nzuri. Kama unavyoona hapa ndio kwake, lakini sisi watoto wake tumejenga tumemzunguka, wote tunaishi sehemu moja, kwa hiyo ukitaka kutoka barabarani ilikuwa ni lazima tupitie kumwona.

"Miongoni mwa vitu tutakavyomkumbuka ni ucheshi wake, kwa sababu tulikuwa karibu naye, ilikuwa rahisi kuja kuleta hata wajukuu hapa kuongea naye, alikuwa ni rafiki yetu," alisema.

Msemaji wa Familia hiyo, Alex Mrema, alisema kaka yake alikuwa anasumbuliwa na ugonjwa wa mapafu na alilazwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili Agosti 15 mwaka huu alikokuwa akipatiwa matibabu na kufariki dunia Agosti 21.

Alisema kaka yake atazikwa keshokutwa katika Kijiji cha Kiraracha, Marangu Magharibi mkoani Kilimanjaro na kabla ya hapo, kesho mwili wake utaagwa nyumbani kwake Salasala, Kinondoni saa tano asubuhi na kisha kufanyiwa ibada katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Augustino saa saba mchana.

"Taratibu za maziko zinaendelea vyema. Kabla ya maziko yake, atapelekwa katika Kanisa la Bikira Maria, Malkia wa Rozari Takatifu Uomboni kwa ajili ya ibada ya maziko.

"Hivi sasa kuna vikao vingine vinaendelea Dar es Salaam na leo jioni (jana), tutafanya kikao hapa nyumbani kwake Kiraracha," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alisema msibani jana kuwa watamkumbuka Mrema kama mpenda amani na mhamasishaji wa maendeleo kwa mkoa huo.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, alisema wanaoingia kwenye siasa wanapaswa kujifunza kutoka kwa Mrema.

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya, Sabina Ntobi (TUDARCo) na Mary Mosha (MOSHI)**

HABARI KITAIFA

# Mtoto wa Simbachawene kupanda kizimbani kesho



**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema linatarajia kumfikisha mahakamani kesho mtoto wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene (pichani) ambaye kwa sasa yuko nje kwa dhamana.

Juzi kwenye mitandao ya kijamii ilisambaa video inayomwonyesha James Simbachawene, akitoa lugha chafu mbele ya askari wa usalama barabarani, huku ikidaiwa kwa sakata hilo lilitokea baada ya kuzidiwa na ulevi na kugonga gari zaidi ya moja na kuendelea na safari bila kujali.

Video nyingine ilisambaa ikionyesha watu wanaolalamikia magari yao kugongwa na kijana huyo aliyekuwa akijitapa kuwa hawezi kufanywa chochote kwa kuwa yeye ni mtoto wa waziri.

Akizungumza na Nipashe jana Kamishna Msaidizi wa Polisi Kanda Maalum, William Mkonda, alisema wamepeleka jalada lake kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwamba likirudi wanatarajia kumpeleka mahakamani Agosti 24, mwaka huu.

"Alikuwa anashikiliwa, lakini ameshaachiwa kwa dhamana kwasababu ni haki yake ya msingi na tulipeleka jalada leo (jana), lakini halijarudi mapema hivyo tunatarajia kuendelea na taratibu zingine za kumfikisha mahakamani Jumatano," alisema Mkonda.

Kutokana na tukio hilo, wananchi wamekuwa wakitoa maoni mbalimbali baadhi wakionyesha kumuunga mkono Waziri Simbachawene kwa msimamo alioutoa.

Mmoja wa wananchi waliotoa maoni katika ukurasa wa Facebook wa gazeti hili kuhusu sakata hilo, Flory Kayjage, alimsifia waziri Simbachawene akisema ameonesha mfano mzuri kwa Watanzania huku akitoa wito kwa viongozi wengine kuiga mfano huo.

Ismail Ibrahim, alidai kuwa watu wenye wazazi, ndugu au jamaa wenye vyeo serikalini baadhi wana viburi, huku akikumbushia sakata lililotokea 2016 lililomhusisha mke wa aliyekuwa Waziri Dk. Agustino Mahiga na askari, baada ya kumwandikia faini dereva wake kwa kosa la kutosimama sehemu ya kuvuka watembea kwa miguu.

Naye Bint Qaseem H, alisema hiyo ni kwa faida ya kijana huyo, akidai kuwa itamfunza adabu na kujua kuwa mtoto wa mkubwa anapaswa kuishi vipi, huku Oscar Mwambene akiandika "Safi waziri mtoto lazima awe na adabu na watu wengine," alisema.

Kwa upande wa Iddi Mpore, alishauri kuwa sheria iachwe ichukue mkondo wake "Asije akaonekana mtaani mkaanza kulaumu, hapana huenda kamudu kulipia adhabu inayotoka kwani ina kifungo au kulipa faini," alisema na kuongeza;

"Huyo sio mtoto wa kigogo wa kwanza kuyafanya hayo bali ni mihemko tu ya watu inafanya aonekane kama yeye mwanzilishi wa hayo makosa, tuache sheria ifuate mkondo wake," alisisitiza Mpore.



Mbunge wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo (katikati), akizungumza na baadhi ya wakazi wa kisiwa cha Rukuba juzi, kwa ajili ya kuhamasisha sensa inayofanyika leo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango ataka ushirikiano malezi, maadili ya watoto

**Na Beatrice Shayo**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philipo Mpango, amewataka wazazi, walezi, walimu na wadau mbalimbali kushirikiana kurudisha maadili na malezi bora kwa watoto na kuendelea kupinga vitendo vya ukatili dhidi yao.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika Mkutano Mkuu wa 13 wa Jumuiya ya Skauti Wakike Tanzania (TGGA) uliohusisha nchi 33 kutoka Bara la Afrika kwa lengo la kuthamini hatua walizopiga miaka mitatu iliyopita, tathmini ya changamoto ya janga la UVIKO-19 na kuchagua uongozi mpya.

Dk. Mpango aliwasihi wanachama wa chama hicho kuendelea kushirikiana na serikali zao pamoja na jamii kwa ujumla hasa katika kipindi hiki cha utandawazi katika kusimamia malezi ya watoto.

Alisema vitendo vingi vya kikatili vinavyoendelea kufanyika ni kwasababu wazazi na walezi wengi hawaongei na watoto wao kujua matatizo wanayokabiliana nayo.

"Vitendo vya kikatili vinaendelea kufanyika kwa sababu sisi kama wazazi na walezi hatuongei na watoto wetu, umefika wakati lazima tukemee vitendo hivi bila uwoga na hatua za kisheria zichukuliwe kwa wahusika wote wanaofanya vitendo vya kikatili," alisema.

Alisema kwa sasa malezi ya watoto yapo katika mikono ya dunia na ili kufanikiwa kuwa na ulezi bora na kulinda mustakabali wa watoto jamii haina budi kushirikiana kwa pamoja kama kaulimbiu ya chama hicho kinavyosema "Tustawi pamoja rudisha mustakabali wa bara la Afrika kwa kutumia maarifa, ujuzi na vipaji vya wanawake vijana".

"Ni vyema tustawi pamoja na kuacha alama, ni lazima sote tutembee pamoja tushirikiane wanawake kwa wanawake, pia wanawake na wanaume kuhakikisha watoto wetu tunawalinda."

Alisema hiyo ndiyo njia pekee ambayo wazazi na walezi wanapaswa kuitumia kuhakikisha watoto wanatumia maarifa, ujuzi na vipaji vyao kwa maendeleo ya Bara la Afrika na Tanzania.

Alisema mmomonyoko wa maadili una athari zake katika nchi za Afrika na kusababisha kurudisha nyuma jitihada za maendeleo na kufanya umaskini uendelee.

Kwa upande wake, Kamishna Mkuu wa Jumuiya TGGA, Wakili Mary Richard, alisema mkutano huo ni wa kikatiba unaofanyika kila baada ya miaka mitatu wenye lengo la kufanya tathmini na kuweka mikakati mipya ya kuimarisha ushirikiano kwa kuangalia changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi na kutoa elimu ya lishe bora.

Alisema chama chao kimeendelea kutoa mafunzo kwa watoto wa kike hasa kutatua changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi na kutoa elimu ya lishe bora.

SOS CHILDREN'S VILLAGES

**CONSULTANCY SPECIAL ASSIGNMENT**

SOS Children's Villages Tanzania is a local non-government organization affiliated to SOS Children's Villages International, a worldwide child care and protection organization that provides orphaned and destitute children with a permanent home and educational opportunities. Established 60 years ago, SOS Children's Villages International the umbrella organization currently has Children's Villages and other projects in 135 countries around the world. Globally, it runs the SOS Children's Village Programme which has two main arms, i.e. Family Based Care based at SOS Children's Villages and Family Strengthening Programmes supporting families in local communities. SOS has been working in the United Republic of Tanzania since 1991 and implements its programs in the following locations Zanzibar, Arusha, Dar es Salaam, Mwanza, and Iringa. SOS Children's Villages Tanzania seeks to recruit suitably qualified Consultant to carry out the Special assignment as per the below requirements:

**Task: Support Family Strengthening Program Exit Process in Arusha District Council**
**Start date:** 01 Sept 2022
**End date:** 31st December 2022
**Report to:** Program Manager (Overall) and Senior FS Coordinator (Technical)

**Overall Objective of the Assignment**

The main objective of this position is to facilitate a smooth exit process of the Family Strengthening program in 17 wards of Arusha District Council by planning, monitoring, and producing comprehensive reports that entail those beneficiaries for transition to other programs as well as graduation for those beneficiaries attained self-reliance.

**Specific Responsibilities**

- Facilitate household/Family capacity assessment for beneficiaries' graduation & transition and prepare a family capacity assessment report
- Facilitate Exit meeting with Arusha LGAs on FS program exit
- Facilitate Stakeholders mapping exercise for beneficiaries' transition and graduation and prepare Stakeholder's mapping report
- Facilitate handing over of transitioning beneficiaries to other stakeholders for continued support
- Conduct workshops with government officials on FS Exit strategy and develop a joint action plan for beneficiaries' transition and graduation
- Develop or adopt SOP Criteria and tools for beneficiaries' transition and graduation
- Conduct final meetings for beneficiaries' transition and graduation
- and formal Ensure informing all beneficiaries and stakeholders on the FS Programme phase out in Arusha DC
- Process and provide iCHF cards to families (iCHF) in Arusha District Council
- Ensure monthly allowance for EEWs/CCWs/para-social workers is paid timely
- Conduct Jointly supervision support with Arusha District Council officials on monitoring and follow-up program exit activities
- Prepare monthly progressive reports
- Preventing and mitigating all possible risks in the area of child protection and Safeguarding
- Reporting immediately on any issue related to Child abuse/ violence/ neglect/ mistreatment.

**Required Qualification, Skills, and Experience**

- Bachelor/or higher degree in Sociology, Social Work, Community Development, Project Management, Statistics, and any other relevant field from recognized institutions.
- At least five years of working experience preferably with an NGO in this field.
- Basic facilitation skills.
- Basic skills in data collection, collation, analysis, interpretation, and report writing
- Basic Knowledge of Gender, Child rights, and Advocacy.
- Ability to work with minimum supervision.
- Computer skills especially Microsoft word, Excel & the Internet.
- A good command of both oral & written English

**How to apply:**

Interested candidates for the above position should submit an application letter by email enclosed with only a detailed and updated CV with telephone contacts, email address, and details of at least 3 referees. Only contacted candidates for the interview will submit copies of academic and professional certificates. This advert can be obtained on our website **http://www.sos-childrensvillagestanzania.or.tz**. The closing date is **31st August 2022.** To apply please send to;

**The National Director SOS Children's Villages Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania**
**recruit.sostanzania@sos-tanzania.org**

**Please Note:** SOS Children's Villages Tanzania is an equal opportunity employer and committed to keeping children safe from abuse and harm, therefore candidates applying for this post will be subject to child safeguarding recruitment procedures and checks.

217007601

SIMULIZI MAISHA YA MREMA

# Mwinyi, Mkapa waeleza Mrema alivyowasumbua

**Na Salome Kitomari**

RAIS wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amebainisha uhodari wa Augustino Mrema na namna alivyokipa shida Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Uchaguzi Mkuu wa kwanza wa vyama vingi mwaka 1995.

Kupitia kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anaeleza namna alivyomtumia Mrema kuwashughulikia viongozi walioamua kuandamana bila kufuata sheria, akiwamo mwanasheria nguli Mabere Marando mwanzoni mwa miaka 1990, kipindi hicho Mrema akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mwinyi aliyeongoza Tanzania kuanzia mwaka 1985 hadi 1995, ndiye alimteua Mrema kuwa Naibu Waziri Mkuu, cheo ambacho hakiwapo kikatiba na anakiri kujuta kuchukua uamuzi huo japo aliufanya kwa nia njema.

"Lakini wakati mwingine tunashindwa kuelewa watu wengine wana shida gani, pamoja na uamuzi wa CCM na serikali, bado baadhi waliotamani kuanzisha vyama vya siasa hawakutaka kusubiri mjadala wa kitaifa ukamilike na mfumo wa kisiasa ubadilishwe kwa mujibu wa sheria kabla ya kuanzisha fukuto la vyama vingi na hata kuthubutu kuanzisha vyama.

"Miongoni mwa waliotusumbua sana walikuwa Chifu Abdallah Fundikira, Osca Kambona, Seif Sharrif Hamad, James Mapalala na Mabere Marando, walijaribu kufanya fujo sana ikiwamo kuandamana bila kibali, lakini wakati ule nilikuwa na Waziri Mrema ambaye aliwadhibiti ipasavyo," Mwinyi anasimulia.

Anasema baada ya hapo ilibidi CCM izinduke na kuanza kutafuta wanachama wengi zaidi kabla vyama vingi havijaruhusiwa.

Katika ukurasa wa 269 wa kitabu chake hicho, Mwinyi anasema kuwa baada ya kuanzisha upinzani nchini, hakuwa na wasiwasi na hiyo ilikuwa kabla Mrema hajahamia upinzani, lakini mambo yalibadilika kutokana na uamuzi wake huo anaokiri uliwasumbua na 'kuwachangamsha kidogo'.

Anakumbusha kuwa Januari 24, 1993 alimteua Mrema kuwa Naibu Waziri Mkuu, cheo ambacho hakikuwapo kikatiba, lakini alichokusudia ni kutambua utendaji wake na mchango wake katika kuifanya serikali iwe karibu na wananchi na kutatua matatizo yao kwa haraka.

"Alijitosa kusukuma ujenzi wa vituo vya polisi, alisikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi, mara nyingi akiagiza hatua zichukuliwe ndani ya siku saba. Kwa mfano nilivutiwa sana na jinsi alivyofanikiwa kumaliza mgogoro wa ardhi wilayani Arumeru uliohusu Dayosisi ya Meru na iliyokuwa Dayosisi ya Mlima Meru zote za Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania uliodumu kwa miaka miwili na kuhatarisha hali ya amani na utulivu eneo hilo.

"Ugomvi huo ulisababisha vifo na uharibifu wa mali. Kwa kweli nilifurahi sana kuona amefanikiwa kuumaliza na baada ya hapo ndipo nikampa nafasi hiyo ya Naibu Waziri Mkuu.

"Waswahili husema 'unadhani umepata kumbe umepatikana', nilikumbuka msemo huo miezi kadhaa baada ya kumteua kuwa Naibu Waziri Mkuu. Huo ulikuwa uamuzi ambao baadaye nilikuja kuujutia sana," Mwinyi anakiri.

Anasema katika kumteua lengo lilikuwa kumpa madaraka ya kufanya aliyoanza kuyafanya kupambana na rushwa na uonevu.

"Kumbe mwenzangu alikuwa na mahesabu tofauti. Mrema aliwahi kuwa Ofisa Usalama wa Taifa na alisomea propaganda na uenezi Bulgaria, na ni wazi alihitimu vizuri somo hilo. Alikuwa mjanja sana," anasema.

Mwinyi anasema kuwa mwaka 1982, Mrema alikuwa miongoni mwa maofisa walioendesha semina za chama za uchaguzi na baada ya kazi hiyo, wenzake walirejea Dodoma, lakini yeye aliomba kubaki kwa ajili ya kazi ya zaidi kwenye Jimbo la Moshi Vijijini.

"Kumbe alikuwa anajiandaa kugombea jimbo hilo, akalizunguka lote kabla ya wakati wa uchaguzi. Uchaguzi ulipokuja, akagombea na kushinda, lakini matokeo yalipingwa mahakamani, mwaka 1987 akashinda kesi akawa mbunge.



"Mwaka 1990 akagombea tena jimbo hilo akashinda, nami (Mwinyi) nikamteua kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Mwaka 1991 ulikuwa hukosi kumsikia Mrema akifanya vitu vyake karibu kila siku. Kwenye magazeti alisikika kuliko Rais.

"Nilipomteua nilimtaka awe hodari kupambana na maovu na nikaagiza apewe ulinzi wa ziada. Yeye mwenyewe alipoulizwa iwapo haogopi kuuawa, alisema anaamini Mwenyezi Mungu atamlinda, lakini kwamba yuko tayari kufa kwa ajili ya Watanzania," Mwinyi anasimulia.

Anasema Mrema alifanya mengi na kujizolea sifa na wakati mwingine aliingilia hata mambo ambayo si ya wizara yake, lakini aliendelea kumvumilia kwa kuwa alisaidia kuonyesha serikali haijalala, iko macho na alikuwa hodari wa kauli za vichekesho, baadhi ya marafiki zake walimwambia alienda kasi sana na angekwama muda si mrefu.

"Aliwajibu kwamba nilipompa kazi hiyo sikumwambia aende spidi gani... alikuwa tishio kwa wafanya dhuluma ingawa naye aliwahi kukiri wapo walioonewa katika juhudi zake... mwaka 1995 sikuona uwezekano wake wa kugombea urais kupitia CCM.

"Akaamua kujiuzulu uwaziri na kisha baada ya mwezi mmoja akahamia NCCR-Mageuzi, wakampa uenyekiti na kumtangaza kuwa mgombea urais wao. Chama hicho kilijaa wasomi hasa wanasheria wasiokuwa na uzoefu wa siasa, hivyo walimkaribisha Mrema wakimwona ana mvuto kwa wananchi,"anasema Mwinyi katika ukurasa wa 271.

Aliwataja waliokuwa kwenye chama hicho ni Marando, James Mbatia, Masumbuko Lamwai na Prince Bagenda na kwamba iliwasumbua sana CCM kutokana na kwamba alisomea na kuhitimu vyema propaganda, lakini chama kilifanya kazi kubwa wakashinda.

Hata hivyo, Mwinyi ana angalizo lake kwamba kama uamuzi wa kuhamia NCCR-Mageuzi ungefanyika siku chache kabla ya uchaguzi, basi isingekuwa rahisi kwa CCM kumshinda.

"Nikiangalia nyuma ninaona Mrema pamoja na ujanja wake wote, hakuwa na mkakati mzuri. Kwa maoni yangu Mrema ni hodari wa mbinu kwenye medani lakini siyo mpanga mikakati hodari.

"Baada ya kutambua kuwa hawezi kuwa mgombea wa CCM huku akijiamini kuwa ni maarufu, alikurupuka kujitoa CCM. Angesubiri na kujitoa karibu zaidi na uchaguzi tusingepata muda wa kutosha kumshughulikia," anasema.

**MKAPA**

Vilevile, Rais wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa, katika kitabu chake cha 'My Life My Purpose' (Kusudio la Maisha Yangu) ukurasa wa 109 hadi 110, anaeleza namna uchaguzi wa mwaka 1995 ulivyokuwa mgumu na walivyofanikiwa kumshinda Mrema.

Mkapa anakiri Mrema aliwasumbua kutokana na uamuzi wa haraka usiokuwa, lakini akiutafsiri kwamba haukuwa na busara.

Anasema Mrema alikuwa ameshawahi kuwa kiongozi mwandamizi serikalini, hivyo alijua kazi za serikali na aliwahi kwa wananchi kama namna ya kujikinga, akiwa makali kwa jamii ya watu wenye asili ya India ambao walikamatwa hata kama hakuwa na madaraka hayo.

"Jamii ilimwona kama mtu imara sana anayeweza kuipeleka nchi mbele kutokana na kusambaa taarifa kuwa serikali ya CCM haikuwa inafanya vizuri, chama kiliogopa huenda wananchi wangemchagua Mrema.

"Baadhi ya watu walisema hatumjui Mkapa, tunajua alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje na hajui siasa," Mkapa anasimulia kupitia kitabu chake hicho.

Anasema kuwa kutokana na hali hiyo, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kwa mara ya kwanza, akalazimika kushiriki kikamilifu kumpigia kampeni kumnadi kwa wapigakura na hatimaye akashinda uchaguzi huo.

Mrema alifariki dunia juzi asubuhi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alikokuwa anapatiwa matibabu.

# Upelelezi waiva kesi ya kujipatia milioni 105/-

**Na Grace Gurisha**

UPELELEZI wa kesi ya kujipatia Sh. milioni 105.9 kwa njia ya udanganyifu kutoka Kampuni ya Bima ya Alliance inayowakabili wakazi 10 wa Dar es Salaam, akiwamo mwanafunzi, umekamilika.

Mbali na mwanafunzi huyo (Grace Runyoro), washtakiwa wengine ni mama lishe, wapishi, wakili, wafanyabiashara na wajasiriamali, ambapo wana mashtaka 10 ya kujifanya wanufaika wa bima wakati siyo kweli.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Judith Runyoro (41), Stanley Malayi (30), Mwanaidi Isinda, Neema Mtawa (29), Martha Wambura (33), Theresia Masawe (28), Nyemo Malayi (34), Amos Masala (32), Runyoro (24), William Charles (32) na George Mkangala (40).

Taarifa ya kukamilika kwa upepelezi wa shauri hilo ilitolewa jana na Wakili wa Serikali, Ashura Mzava, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate.

Wakili huyo alisema upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuiomba mahakama ipange tarehe ya washtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

Hakimu Kabate aliahirisha kesi hadi Septemba 29, 2022 ambapo washtakiwa watasomewa maelezo hayo. Dhamana yao inaendelea.

Inadaiwa washtakiwa hao walitenda makosa hayo kati Januari 2018 na Mei 2021, ambapo katika shtaka la kwanza, wote pamoja na watu wengine ambao hawapo mahakamani, wanatuhumiwa kula njama ya kutenda kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Washtakiwa wote wanatuhumiwa kujipatia fedha kutoka Kampuni ya Alliance Insurance Corporation Ltd kwa kulaghai na uongo kwamba wao ndiyo wanufaika wa bima huku wakijua siyo kweli.

Mshtakiwa Judith anatuhumiwa kujipatia Sh. milioni 53.5, Stanley anadaiwa alijipatia Sh. milioni tano, Isinda Sh. milioni 4.5, Mtawa Sh. milioni 9.5, Wambura Sh. milioni 6.5, Masawe Sh. milioni tano, Masala Sh. milioni 11.2 na Grace Sh. milioni 5.7, mali ya Kampuni ya Alliance.

# Dhamana madereva 14 yabishaniwa mahakamani

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeeleza kuwa, madereva 14 wanaotuhumiwa kuhamasisha mgomo kama wakipewa dhamana wataingilia upelelezi wa kesi hiyo na kuhatarisha maisha yao kwa kuwa kuna watu wengine 51 hawajakamatwa.

Wakili wa Serikali, Caroline Materu, alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Romuli Mbuya, wakati kesi hiyo ilipoletwa kwa ajili ya usikilizwaji wa maombi ya dhamana ya washtakiwa hao.

Wakili Materu, aliomba mahakama hiyo itumie kiapo cha SSP, Rogasian Wenga ambaye ni Naibu RCO wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam kinachopinga dhamana ya washtakiwa hao kwenye mawasilisho yake mahakamani.

Alidai, upelelezi wa kesi hiyo unaendelea na kama washtakiwa hao wakipewa dhamana wakawa uraiani, wataingilia upelelezi huo.

Pia alidai washtakiwa wakiwa nje kwa dhamana, watahatarisha maisha yao kwa sababu kuna watu wengine 51 hawajakamatwa.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa Washtakiwa hao, Mohammed Majaliwa, alidai kuwa, Wakili Materu hakueleza kiapo hicho cha SSP Wenga, kiliwasilishwa mahakamani hapo chini ya kifungu gani cha sheria.

Pia alidai sheria imetoa nguvu kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuzuia dhamana ya washtakiwa na siyo kwa mtu mwingine yeyote, hivyo, kiapo hicho kipuuzwe kwa sababu hakina msingi wowote wa kisheria.

"Tunaomba mahakama itoe dhamana kwa washtakiwa kwa sababu mashtaka yao yanadhaminika. Washtakiwa ni watu wazima na familia zao, wanaweza kujilinda wenyewe na pia wakili kashindwa kuithibitishia mahakama ni vipi wataingilia upelelezi," alidai Wakili Majaliwa.

Baada ya hakimu kusikiliza hoja hizo, aliahirisha kesi hiyo kwa ajili ya kuandaa uamuzi kama atatoa dhamana kwa washtakiwa au la.

Madereva hao ni Goodlove Materu (42), mkazi wa Tunduma; Shubert Gamuhangibe (43); Issa Kazembe (50); Paul Mwamtekele (42); George Mgoba (36); Hussein Amini (31); Hussein Fokoyo (36); Rajab Malupu (32).

Wengine ni Shida Mazoya (42); Domonic Mrope (47); Buruan Selemani (42), mkazi wa Tunduma; Ramadhani Butera (32); Noah Mwalonde (31); Muhsuni Barua (33); na mfanyabiashara Julieth Kwayi (37), ambao wanatuhumiwa kwa mashtaka manne.

Mashtaka hayo ni kula njama, kushawishi madereva kugoma mgomo na kufanya mkusanyiko usio halali. Inadaiwa tarehe isiyofahamika Mei, 2022 na sehemu mbalimbali zisizofahamika ndani ya Tanzania, waliongoza genge la uhalifu kwenye kundi la WhatsApp lenye jina la 'Kamati ya Roho Mbaya'.

Inadaiwa kati ya Aprili 23, 2022 na Julai 20, 2022 kupitia kundi hilo, wakiwa ndani ya Tanzania na watu wengine ambao hawapo mahakamani, waliwashawishi madereva na malori na kutenda kosa la mkusanyiko usio halali na mgomo.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONYESHA NIA: USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KUREJESHA MBINU ZA KUPATA MAHITAJI YA MAISHA KUPITIA UENDELEZAJI WA UJASIRIAMALI.**
**REJEA: 0010007865**

EACOP Ltd (Kampuni) Tanzania, kampuni ya mafuta na Gesi, inaalika taasisi zenye uzoefu na sifa kuonyesha nia ya kutoa huduma ya kuandaa, kusimamia na kutekeleza ''Programu ya Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha Kupitia Uendelezaji wa Ujasiriamali'' ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

EACOP na serikali ya Tanzania wametwaa ardhi kwa ajili ya mradi. Mradi huu umeandaa Mipango Kazi ya Uhamishaji watu na Makazi (Resettlement Action Plans) kwa ajili ya vipengele tofauti tofauti au mikoa inayoguswa na mradi (zinapatikana kwenye tovuti ya EACOP: https://eacop.com/information-center/other-publications/).

Mradi upo kwenye hatua za mwisho za uandaaji wa mpango kazi wa uhamishaji watu na makazi wa ziada kwa ajili ya eneo la kituo cha kuhifadhia vifaa kilichopo baharini Tanga. Kila Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi umejumuisha mpango wa Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha (Livelihoods Restoration Plan) na maelezo ya shughuli nane za urejeshaji wa mbinu za kupata mahitaji ya maisha Shughuli namba 7 (Uendelezaji wa Ujasiriamali) ndani ya Mpango wa Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya

Maisha ina lengo la kusaidia kaya zilizoguswa na mradi kuweza kufanya yafuatayo:

- Kutambua fursa za kuendeleza au kukuza biashara ndogo na za kati zinazowekana kufanywa
- Kupata ujuzi wa msingi pamoja na wa hali ya juu wa Uendelezaji wa Ujasiriamali na uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi (haswa kwa wajasiriamali waliopo sasa na wale wenye uwezekano wa kuwa wajasiriamali baadaye, ambao huwenda hawana ujuzi wa ujasiriamali na mawazo ya biashara wakati huu)
- Kufikia fursa za masoko kwa ajili ya biashara mpya na zilizopo
- Kutambua fursa za mafunzo na ujenzi wa uwezo kwa ajili ya kaya zilizoguswa na mradi ili kuhimiza uwezo wao wa kufikia fursa za masoko
- Kutambua fursa za kupata fedha za kuwekeza kwenye biashara ndogo ndogo za kaya zilizoguswa na mradi

Walengwa wa shughuli hizi ni kaya zilizoguswa na wa Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki zilizoko katika vijiji 231 na ambazo ardhi zao zilitwaliwa. Kilimo ndio mbinu tawala ya kupata mahitaji ya maisha katika maeneo yaliyoguswa na mradi. Mbinu kuu ya kaya zilizoguswa na mradi ya kupata mahitaji ya maisha ni kilimo cha kujikimu, pamoja na takribani nusu ya kaya zote kufuga mifugo, kiwango kikubwa cha wafugaji wakiwa katika mikoa kama Dodoma.

Mradi unatafuta taasisi yenye sifa na uzoefu wa kuandaa na kutekeleza programu za aina hii za uendelezaji wa ujasiriamali ili ifanye nayo kazi hizo. Taasisi itakayochaguliwa itahitajika kuwepo eneo la mradi kushirikiana moja kwa moja na wadau na na kaya zilizoguswa na mradi chini ya usimamizi na muongozo wa timu ya mradi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

1. Uthibitisho wa usajili kama shirika/taasisi ambayo shughuli zake zinahusiana na uendelezaji wa ujasiriamali/uboreshaji au urejeshaji wa mbinu za kupata mahitaji ya maisha ndani ya Tanzania.
2. Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
3. Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa kutekeleza programu za uendelezaji wa ujasiriamali vijijni, usimamizi wa programu kubwa za maendeleo na kufanya kazi kwa kushirikiana na sekta binafsi na serikali za mitaa. Wasilisha mifano ya kazi zinazoonyesha uzoefu wa kufanya kazi zinazofanania na hizo zilizofanywa kipindi cha karibuni, ndani miaka mitano iliyopita toka siku ya tangazo hili
4. Wafanyakazi wataopendekezwa kufanya kazi kwenye mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
5. Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi au udhibitisho kuwa wa maombi ya kusajiliwa katika kanzi data yameidhinishwa wakati wa kuwasilisha ombi la kuonyesha nia.
6. Mwombaji azingatie Kanuni ya Sekta ya Petroli ya Ushirikishwaji wa Wazawa/Ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe **20 Mb**) saa au kabla ya saa **11:00** saa za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **5 Septemba 2022.** Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni **0010007865.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

217006101

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Leo ni Siku ya Sensa tujitokeze kuhesabiwa

**LEO** ni siku muhimu kwa Watanzania wote wapenda maendeleo kushiriki kwa kutoa ushirikiano wa kuhesabiwa kwenye Sensa ya Watu na Makazi.

Kutokana na umuhimu wa siku hii, Rais Samia Suluhu Hassan, alitangaza rasmi kuwa ni siku ya mapumziko ili kila mwananchi aweze kushiriki kuhesabiwa.

Serikali na wadau mbalimbali wamehamasisha wananchi kutoa ushirikiano wa kuhesabiwa ili iweze kujua idadi ya watu wake na mahitaji yao kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Maandalizi yote ya kufanikisha siku hiyo yamekwenda vizuri na tumeelezwa kuwa yamekamilika kwa asilimia 100.

Makarani wa sensa, wameshapangiwa vituo vyao vya kutembelea wananchi kwenye mitaa na makazi yao na kwa mujibu wa elimu waliyopatiwa, hawaruhusiwi kutoa siri za taarifa zitakazotolewa na wananchi.

Upungufu wowote uliojitokeza wakati wa maandalizi bila shaka umefanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi ili siku hiyo kusiwe na kisababishi chochote cha kukwamisha zoezi hilo.

Zoezi hili litahusisha ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa wananchi wote kwa maana ya wanawake na wanaume, watoto na watu wazima, wenye ulemavu na wasio na ulemavu. Na litafanyika pande zote mbili za Muungano kwa maana ya Tanzania Bara na Visiwani.

Takwimu zitakapopatikana katika zoezi la sensa zitasaidia kuboresha huduma mbalimbali za wananchi kuanzia sekta ya afya, elimu, maji, umeme na nyingine muhimu kwa jamii.


Kwa mfano, takwimu za sensa zitasaidia Wizara ya Afya katika kuandaa sera na mipango ya afya inayolingana na idadi ya watu katika eneo husika kwa kuzingatia mahitaji yao ya huduma hiyo. Mfano kwa kujua idadi na umri wa watoto nchini na hali zao za kiafya wizara itaweza kuandaa mpango wa kuagiza/kununua idadi na aina ya chanjo kuendana na idadi ya umri halisi wa watoto katika nchi nzima au wilaya husika. Wananchi pia waelewe kuwa mipango yote hupangwa kwa kutumia takwimu za sensa na pia utoaji huduma za afya huendana na takwimu zinazotokana na zoezi hilo. Mfano

ujenzi wa hospitali ya wilaya katika kata eneo husika huhitaji idadi ya wakazi wasiopungua 80,000. Takwimu za sensa pia zitasaidia Wizara ya Elimu kujua viwango vya elimu vya Watanzania wote na kuandaa sera na mipango ya elimu kulingana na idadi, viwango vya elimu na mahitaji ya kielimu ya watu katika eneo husika.

Wizara ya Elimu nchini ipo katika mchakato wa mabadiliko ya mitaala ya elimu ili kuendana maendeleo ya sayansi na teknolojia na mahitaji ya wakati uliopo. Takwimu hizi za sensa zitasaidia utekelezaji wa mchakato huo muhimu unaotegemewa kuleta mabadiliko na maendeleo makubwa katika sekta ya elimu nchini. Mfano kwa kujua idadi ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika, wizara inaweza kuandaa mpango maalumu kwa kuanzisha masomo ya watu wazima nchini ili kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika kwenye jamii. Pia idadi kubwa ya watoto katika eneo husika itaonesha uhitaji wa kuongeza madarasa na walimu zaidi kulingana na idadi ya watoto iliyopo. Wananchi waelewe kuwa mipango na utoaji huduma za elimu nchini hufanywa kwa kuzingatia takwimu za sensa.

Hizo ni baadhi tu ya faida ya sensa katika kuandaa mipango ya maendeleo, hivyo wananchi wanapaswa kuelewa umuhimu wa kushiriki kuhesabiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ndivyo sensa ilivyo muhimu kwa elimu

Na Pankras Luoga

**KUJUA** idadi ya watu, viwango vya elimu na mahitaji yao kielimu ni msingi wa kufikisha huduma bora za elimu kwa kila mwananchi. Leo ikiwa ni Siku ya Sensa ya Watu na Makazi, ni muhimu kwenye elimu ili kukusanya taarifa mbalimbali zikiwamo uchumi, makazi, nishati na elimu kutoka kwa wananchi wote.

Ni muhimu wananchi wakazijua faida za takwimu zitokanazo na sensa katika kuboresha upatikanaji na utoaji wa huduma zote zikiwamo za elimu.

Kwa kifupi kujua faida hizo ni muhimu ili kuongeza uelewa na hamasa ya wananchi kushiriki sensa kikamilifu na kutoa taarifa za kweli.

Baadhi ya faida za sensa katika kuboresha elimu ni pamoja na takwimu za sensa zitasaidia Wizara ya Elimu kujua viwango vya elimu vya Watanzania wote na kuandaa sera na mipango kulingana na idadi, viwango vyao na mahitaji ya kielimu ya watu.

Tukumbuke kuwa kipindi hiki Wizara ya Elimu ipo katika mchakato wa mabadiliko ya mitaala ya elimu ili kuendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia na mahitaji ya wakati uliopo.

Hivyo, takwimu hizi za sensa zitasaidia utekelezaji wa mchakato huo muhimu unaotegemewa kuleta mabadiliko na maendeleo makubwa katika sekta ya elimu. Mfano kwa kujua idadi ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika, wizara itandaa mpango maalumu kwa kuanzisha masomo ya watu wazima ili kupunguza idadi ya wasiojua kusoma na kuandika.

Pia, idadi kubwa ya watoto katika eneo flani itaonyesha uhitaji wa kuongeza madarasa na walimu zaidi kulingana na kiwango cha watoto waliopo.

Wananchi waelewe kuwa, mipango na utoaji huduma za elimu nchini hufanywa kwa kuzingatia takwimu za sensa.

**Wito wangu ni kwamba, kutakuwa na faida nyingi zitokanazo na takwimu za sensa katika kuboresha elimu ya Watanzania.**

Mathalani, ujenzi wa shule ya msingi au sekondari iwe vijijini, kwenye kata, wilaya na mijini hutegemea idadi ya watoto wenye umri wa kuanza shule.

Na zaidi, takwimu hizi za sensa kuhusu idadi ya watoto itasaidia sekta ya elimu kupata uwiano wa mgao wa rasilimali kama vile fedha za kuendesha shule kwa ngazi au sehemu inayojengwa.

Mfano katika mgao wa fedha za elimu huzingatia idadi ya wanafunzi katika eneo shule inapojengwa. Mfano shule ya msingi yenye jumla ya watoto 250 haiwezi kupata mgao sawa wa fedha na ile yenye watoto 500 hata kama zote ni shule za msingi.

Na mwisho upatikanaji wa takwimu sahihi za sensa utafanikisha kufanya tathimini na kufuatilia walimu katika jamii hasa kwa kulinganisha idadi ya wananchi waliofikiwa na huduma za elimu kwa kuangalia jumla ya wananchi wa eneo hilo.

Hivyo, takwimu za sensa zitasaidia wizara ya elimu kutoa huduma inayoakisi mahitaji ya elimu ya wananchi katika eneo lao.

Wito wangu ni kwamba, kutakuwa na faida nyingi zitokanazo na takwimu za sensa katika kuboresha elimu ya Watanzania.

Na baadhi ya faida hizo ni kufanya mgawanyo sahihi wa walimu, madarasa na fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za elimu ikiwa ni pamoja na manunuzi ya vifaa, ujenzi wa madarasa, na upanuzi wa shule kulingana na kuongezeka kwa idadi ya watoto.

Utekelezaji kikamilifu wa haya yote hutegemea upatikanaji wa takwimu za sensa, hivyo ni muhimu kila mwananchi ahamasike kwa kushiriki na kutoa taaarifa sahihi bila kuficha kitu chochote leo ili taifa liboreshe elimu.

**Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Afya MUHAS**
**Maoni: 0757645746.**

## LHRC yaja na mapendekezo saba ustawi wa demokrasia

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimetoa mapendekezo saba kwa serikali, ambayo kinaamini yanaweza kusaidia kuimarisha ustawi wa demokrasia ya vyama vingi nchini.

Miongoni mwa mapendekezo hayo ni kutekeleza uamuzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, kwa kuruhusu kuwapo kwa mgombea huru katika uchaguzi kuanzia ngazi ya chini hadi urais.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Anna Henga, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa mwezi wa demokrasia, kuelekea Siku ya Demokrasia Dunia itakayofikia kilele Septemba 15, mwaka huu.

"Pendelezo letu la pili kwa serikali ni kuishauri itekeleze uamuzi wa Mahakama ya Afrika Mashariki kwenye vifungu vya sheria ya vyama vilivyoamuliwa kuwa vinakinzana na mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema Henga.

Kituo hicho pia kinapendekeza kuridhia Mkataba wa Afrika wa Demokrasia na Uchaguzi 2007, huku pendekezo la nne likiwa ni kuifanyia marejeo Sheria ya Haki za Msingi na wajibu wa kisheria (The Basic Rights and Duties Enforcement Act).

Alifafanua kuwa, hatua hiyo itasaidia kuondoa takwa la mtu kuthibitisha ni kwa namna gani ameathirika katika jambo fulani, kwa kuwa takwa hilo linasababisha wananchi kushindwa kutumia uhuru wao wa kidemokrasia.

"Lakini pendekezo letu la tano ni kutaka vyama vipewe uhuru wa kufanya mikutano ya hadhara kwa mujibu wa Katiba, ambayo ilizuiwa tangu mwaka 2016," alisema.

Katika pendekezo la sita, kituo hicho kinataka kuendelea kuruhusu wananchi na wadau mbalimbali kufanya mijadala, makongamano na midahalo ya haki za kidemokrasia.

"Tunapendekeza kuhakikisha Watanzania wanapata Katiba Mpya kabla ya mwaka 2025 kwani Katiba Mpya ni sasa," alisema.

Alifafanua, katika kuelekea maadhimisho ya siku hiyo, kituo hicho kitafanya shughuli mbalimbali ikiwamo utoaji elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuwa na Katiba Mpya.

"Tutatoa elimu kuhusu umuhimu wa wananchi katika haki za kidemokrasia, mjadala wa haki za kidemokrasia, tathmini ya miaka 30 ya siasa za ushindani nchini na mambo mengine muhimu," alisema.

Alisema, kituo hicho kimekuwa na mchango mkubwa wa kukuza na kuimarisha haki za kidemokrasia nchini tangu kuasisiwa kwake mwaka 1995, ikiwa ni pamoja na kufungua mashauri mbalimbali yenye maslahi kwa umma, katika mahakama za ndani kikanda na kimataifa.

# Kiama chaja waagizaji wa kemikali hatarishi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

SERIKALI imetangaza kiama kwa kampuni zinazoingiza madini ya zebaki kinyemela nchini kwa kuwa ni hatari kwa afya za wananchi yasipodhibitiwa.

Kemikali hizo zinachangia kusababisha magonjwa ya mfumo wa fahamu, ini, figo, mfumo wa uzazi pamoja na athari kwa wajawazito na watoto.

Angalizo hilo lilitolewa jana jijini Mwanza na Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelis Mafuniko, alipozungumza na waandishi wa habari.

Dk. Mafuniko alizitaka kampuni zinazotaka kuingiza bidhaa hiyo nchini, zisajiliwe ili zitambulike kisheria na kukidhi matakwa ya Mkataba wa Kimataifa wa Minamata unaohimiza nchi wanachama kulinda afya za wananchi na mazingira dhidi ya zebaki.

"Kuanzia leo (jana) Agosti 22, 2022 serikali inazitambua kampuni 10 zilizojisajili na kufuata matakwa ya serikali kwa ajili ya matumizi ya kemikali za zebaki.

"Kwa watakaotumia kemikali bila kibali na kuthiri mazingira na afya ya jamii, hatutakubali, ndiyo maana tumetoa mwongozo wa matumizi ili kupata mwelekeo wa kuondoa matumizi mabaya ya kitendea kazi hicho," alisema.

Dk. Mafumiko pia alibainisha kuwa tangu Septemba 2021, tani tano za zebaki zilizosajiliwa zimeingizwa nchini huku akiwataka waagizaji kuhakikisha kemikali hiyo inatumika kwa kuzingatia sheria ili kulinda afya za watumiaji.

Alisema serikali inasimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani ya Mwaka 2003 ambayo inaelekeza namna ya kuingiza kemikali hizo nchini.

Dk. Mafumiko alizitaja kampuni zinazotambulika kisheria zitakazohusika na usambazaji na uuzaji wa kemikali hizo ni Tri Star LTD, Waswa Co Ltd, Kadula & Kapata Co. Ltd, Mhange Sungwa Maduhu (Sukachem Traders), Jema Chemicals Co. Ltd, Machugu Investment, Jomaya Enterprises, Mwiwa Co. Ltd na Angelus Albinus Anthony.

Mkuu wa Operesheni wa Kampuni ya Jema Chemicals Co. LTD, Fredrick Otieno, aliiomba serikali kudhibiti matumizi mabaya ya zebaki ili kulinda afya za wananchi.




Wakulima wa Kijiji cha Ntokela, Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya wakiwa na mifuko yenye mbolea aina ya DAP baada ya kununua kwa wakala wa kampuni ya OCP. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima wanufaika na mbolea ya ruzuku

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wa mikoa ya Njombe, Mbeya na Tabora wameanza kunufaika na mbolea ya ruzuku baada ya mpango huo kuzinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima jijini Mbeya.

Rais Samia aliagiza wakulima waanze kunufaika na mbolea ya ruzuku ifikapo Agosti 15, 2022 ili kuwawezesha kuwa nayo wakati wakielekea msimu wa kilimo kwa ajili ya maandalizi.

Taarifa ya kuanza rasmi kwa mauziano ya mbolea hiyo ya ruzuku yametolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stephan Ngailo juzi, jijini Dar es Salaam na kubainisha kuwa mpaka siku hiyo wakulima wa mikoa ya Njombe, Mbeya na Tabora wameanza kuununua mbolea kwa bei elekezi ya ruzuku.

Alisema maeneo mengine yaliyotarajiwa kuuza mbolea ya ruzuku kuanzia jana ni Songea, Mbinga, Lindi na Mtwara huku akitoa wito kwa wakulima kujitokeza kwa wakati kujisajili ili kunufaika na mbolea hizo na kusisitiza hakuna mkulima atauziwa mbolea hizo bila kusajiliwa.

Wakala wa kampuni ya ETG mkoani Tabora, Salum Mchele, alikiri kuwa kilimo cha nyanya na matikiti kinatumia mbolea nyingi na kueleza kuwa msimu uliopita wa kilimo walinunua kwa bei kuanzia Sh. 140,000 hadi 160,000 na kuonesha furaha yake sasa wauzaji wanatekeleza agizo la Rais Samia kwa kuuza bei elekezi ya Sh. 70,000.

Pia, serikali kwa kushirikiana na waingizaji na wauzaji wa mbolea imewataka wakulima kununua mbolea kwa namba za utambulisho walizopewa wakati wa usajili na kutahadharishwa kutoa namba kwa mtu mwingine kununua mbolea hiyo.

Alisema kufanya hivyo hakutafanikisha zoezi la kununua mbolea kwa kuwa namba pekee haimfanyi mkulima kununua mbolea na kueleza vipo vigezo tofauti vinavyoangaliwa kulingana na taarifa zilizopo kwenye mfumo wa uuzaji wa mbolea hizo za ruzuku.

Kuanza kwa uuzaji huo kumetokana na mafunzo ya mfumo wa biashara ya mbolea ya ruzuku kwa mawakala kupitia mfumo wa kidijitali wa ruzuku ya mbolea kwa msimu wa kilimo 2022/2023.

# Hospitali yaidai Wizara ya Afya milioni 460/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

HOSPITALI Teule ya Makiungu iliyopo wikayani Ikungi mkoani Singida inayoendeshwa kwa ushirikiano kati ya Kanisa Katoliki Jimbo la Singida na serikali, inaidai Wizara ya Afya Sh. milioni 466 ambazo ni malimbikizo ya mishahara ya watumishi.

Mganga Mkuu wa Hospitali hiyo, Dk. Emmanuel Chidodolo, alibainisha hayo juzi wakati wa hafla ya kubariki na kufungua majengo mapya ya hospitali hiyo ambayo mgeni rasmi alikuwa Askofu Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mwadhama Kardinali Polycarp Pengo.

"Hospitali inakumbana na changamoto ikiwamo ufinyu wa bajeti katika vyanzo vya ndani na nje ya hospitali, yaani wadau tunaoshirikiana nao ambapo kuna madeni ya muda mrefu ambayo hospitali inaidai Wizara ya Afya Sh. milioni 466 za deni la mishahara," alisema.

Dk. Chidodolo alisema deni hilo ambalo lilishahikikiwa na ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG), halijalipwa kwa muda mrefu na hivyo kukwamisha shughuli za uendeshaji wa hospitali hiyo.

Alisema shida nyingine ni kodi kubwa wanayotozwa wakati wanapoingiza vifaa kutoka nje kwa ajili ya hospitali wakati vifaa hivyo ni kwa ajili ya kuboresha huduma za afya za wananchi.

Dk. Chidodolo aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuipandisha hadhi hospitali hiyo kuwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa kwa kuwa kufanya hivyo kutapanua wigo wa huduma zake kwa wagonjwa.

"Endapo hospitali hii itabaki katika ngazi ya wilaya maboresho ya huduma za afya yanayofanyika hapa, hayatawanufaisha baadhi ya wagonjwa hasa wateja wa bima ya afya," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema serikali itahakikisha inajenga hoja ili Hospitali Teule ya Makiungu iliyoko wilayani Ikungi ipandishwe hadhi na kuwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa kwa lengo la kupanua wigo wa huduma kwa wagonjwa.

"Ninapenda Askofu Jimbo la Singida, Edward Mapunda nikuhakikishie kwa uwezo wa Mungu tutajenga hoja ili hii hospitali iweze kupandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa," alihidi.

Serukamba alilipongeza Kanisa Katoliki kwa jinsi ambavyo limekuwa bega kwa bega katika kusaidia serikali katika sekta ya afya na elimu.

Mkuu wa Mkoa aliwapongeza wafadhili wa nje kupitia Padri Alessandro Nava na Dk. Manuela Buzzi na Shirika la Mapadre Wakonsolata waliosaidia ujenzi wa hospitali hiyo ambao wamekuwa na mchango mkubwa katika Kanisa Katoliki Jimbo la Singida.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro, alisema tangu wilaya hiyo ilipoanzishwa mwaka 2012, serikali imekuwa na ushirikiano mzuri na Kanisa Katoliki Jimbo la Singida katika sekta ya afya, elimu na huduma za jamii.

Hospitali ya Makiungu ilifanywa kuwa hospitali teule mwaka 2008 na Julai 2013 ilimegwa kutoka Wilaya ya Singida Vijijini na imekuwa ikipokea ruzuku kutoka serikalini kwa njia ya Mfuko wa Pamoja (Basket Fund), dawa na vifaa tiba kutoka Bohari ya Dawa (MSD) na baadhi ya watumishi wa hospitali wanalipwa mishahara na serikali.



Mkurugenzi wa Mawasiliano na Jamii wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Neli Msuya (kulia), akitoa maelezo ya shughuli za mamlaka kwa wananchi waliofika katika banda la mamlaka hiyo wakati wa mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Mto Nile uliofanyika jijini Dar es Salaam. Anayeshuhudia ni Meneja Mawasiliano DAWASA, Everlasting Lyaro. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Maboresho elimu kuleta mabadiliko

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema maboresho yanayoendelea kwenye sekta ya elimu nchini, ikiwamo sheria, mitaala na sera yatachangia kwa kiwango kikubwa kuleta mageuzi katika sekta hiyo nchini.

Pia imesema maboresho hayo yatasaidia kuzalisha wahitimu wenye uwezo wa kufanya kazi katika sekta mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar, Lela Mohammed Mussa, alisema hayo jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa pili wa kimataifa wa Elimu Bora (IQEC) ulioandaliwa na Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET) na kukutanisha wadau kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Alisema mabadiliko ya mfumo wa elimu nchini na mitaala ni jambo la muhimu kwa kuwa litasaidia kuimarisha uzalishaji wa rasilimali watu ili kukidhi mahitaji ya sasa ya nchi pamoja na kuwawezesha vijana wa Kitanzania kutambua uwezo wao baada ya kuhitimu masomo yao.

"Juhudi zote za maboresho zinazoendelea, zinalenga kuleta mapinduzi katika mfumo wa elimu nchini, miongoni mwa maeneo ambayo maboresho yanagusa ni pamoja na kwenye mitaala kadhaa ya vyuo vya msingi, sekondari na elimu ya juu," alisema Lela.

"Tunataka mtoto anayemaliza shule aajirike au ajiajiri mwenyewe kwa sababu kilio kikubwa katika elimu ni kwamba wahitimu wengi hawawezi kuajirika au kujiajiri kwa sababu wanakosa ujuzi unaotakiwa."

Alisema, ili nchi ifikie malengo mbalimbali ya maendeleo, kunahitajika juhudi za makusudi kuandaa rasilimali watu yenye uwezo unaohitajika katika soko la ajira.

Alisema pamoja na maboresho yote ambayo serikali inayafanya, bado inaendelea na utekelezaji wa programu mbalimbali za kuwezesha upatikanaji wa elimu bora nchini ikiwamo vifaa kama madawati, vitabu pamoja na kuendelea kuajiri walimu.

Mratibu wa taifa wa TEN/MET, Ochola Wayoga, alisema lengo la mkutano huo ni kujadili kwa kina hatima ya sekta ya elimu na kutoa suluhisho la kuisaidia kukua na kuleta manufaa ndani na nje ya Tanzania.

# Waziri ataka taarifa shule zilizokaidi agizo la serikali

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imewataka wadhibiti ubora wa elimu nchini kufanya uchunguzi wa kina na kutoa taarifa kuhusu shule zilizokiuka maelekezo ya serikali ya kufunga wakati wa likizo.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda, alipozungumza na waandishi wa habari katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MOCU) kuhusu sensa ya watu na makazi inayofanyika leo.

"Serikali ilishatoa maelekezo kuhusu kufungwa kwa shule zote za msingi, sekondari na vyuo nchini kupisha sensa ya watu na makazi inayofanyika leo nchini kote, lakini bado baadhi ya shule wamekaidi maelekezo hayo," alisema.

Waziri Mkenda alisema taarifa za awali zinaonyesha asilimia kubwa ya shule ambazo hazijafungwa hadi sasa ni za taasisi au watu binafsi ambazo zimejipangia muda wa kufunga.

"Wakati wa kujadili utekelezaji wa sensa ya watu na makazi, wenzetu wa shule binafsi walitaka tusiwabane sana, kuwe na fursa ya kutekeleza mpango huo, lakini sasa tumebaini uhuru umekuwa mkubwa na wengine wataharibu sensa, hatutakubali, " alionya.

Prof. Mkenda alisema serikali imepokea taarifa kwamba wapo baadhi ya wamiliki wa shule walitarajia kufunga Agosti 22 mwaka huu, hatua ambayo alisema itakwamisha wanafunzi wanaotoka mikoa ya mbali kushiriki sensa.

"Hebu fikiri kwa mfano shule inafungwa Agosti 22, huyu mwanafunzi anayetoka Dar es Salaam hadi afike Ruvuma au Kagera itamchukua muda gani na changamoto za usafiri njiani? Ninasema wadhibiti ubora wasimamie hilo na shule zifungwe, wanaokaidi leteni taarifa zao," aliagiza.

Prof. Mkenda alisema kuna umuhimu mkubwa wa kutekeleza sensa na kwamba ujenzi wa shule unategemea idadi ya wanafunzi eneo husika, huku akiahidi ushirikiano wa serikali na kuwataka shule binafsi kuheshimu maelekezo ya serikali.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametangaza siku ya sensa ni mpumziko, sasa tufuate agizo hilo... maana sensa itaanza leo, lakini itaendelea baada ya hapo," alisema.

# Vijana wapewa fursa za uchumi wa buluu

**Na Mbaraka Kambona,**
MWANZA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewahimiza vijana wa Kanda ya Ziwa Victoria kufuga samaki ili kujiongezea kipato na kuongeza fursa za ajira nchini.

Waziri Ulega alitoa wito huo kwa nyakati tofauti akiwa ziarani wilaya za Ukerewe na Ilemela, mkoani Mwanza mwishoni mwa wiki.

Alisema serikali imejipanga kutumia fursa za uchumi wa buluu zilizopo ndani ya Ziwa Victoria kuwawezesha vijana kufuga samaki kwa kutumia vizimba na kuuza ndani na nje ya nchi ili kujiongezea kipato.

"Rais Samia ametoa Sh. bilioni 20 kwa ajili ya kuwezesha vijana kufuga samaki katika vizimba, hivyo ni wakati sasa wa kujipanga ili pesa hizo zitakapokuja tuweze kuzitumia vizuri kufanya uzalishaji wa samaki kwa wingi ili tuweze kuuza na kupata kipato," alisema.

Alisema samaki aina ya sato wanahitajika kwa wingi ndani na nje ya nchi, uhitaji ni mkubwa na kuwataka vijana wajipange vizuri ili waweze kutumia fursa hiyo kujiinua kimaisha.

Kwa upande wa vijana wanaojishughulisha na ufugaji wa samaki, Bahati Paul, kutoka Ilemela na Peter Emmanuel kutoka Ukerewe kwa nyakati tofauti walisema kuwa mpango huo wa serikali wa kuwawezesha vijana utasaidia waweze kujiajiri na kuondokana na kero ya ukosefu wa ajira.

Aidha, waliiomba serikali kutatua tatizo la chakula cha samaki ambalo linachangia kuongezeka kwa gharama za uzalishaji.

Katika hatua nyingine, Waziri Ulega alisema mwaka huu pia serikali itawakopesha wavuvi nchini boti za kisasa zaidi ya 150 ili waweze kuboresha shughuli zao na kuongeza uzalishaji wa samaki.

Kadhalika, boti hizo zitafungamanishwa na teknolojia za kisasa zitakazomsaidia mvuvi kurahisisha shughuli za uvuvi.

Waziri Ulega alifafanua kuwa mkopo huo wa masharti nafuu unalenga kuwawezesha wavuvi kuboresha uvuvi wao kwa sababu nia ya Rais Samia ni kuwatoa katika uvuvi wa kuwinda na kufanya wa kisasa wa uhakika.

# Makamba ataka sekta binafsi kuungana uwekezaji nishati

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amezitaka sekta binafsi kuungana na kuwekeza kwenye miradi mikubwa ya nishati nchini badala ya kuwaachia wawekezaji wa kigeni.

Amesema miradi kama ya nishati jadidifu, upepo pamoja na yenye mitaji mikubwa, sekta binafsi wanapaswa kuungana na kufanya uwekezaji kwa maendeleo ya taifa.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam alipokutana na maofisa watendaji wakuu (CEOrt) kutoka kampuni mbalimbali nchini, wakijadiliana kuhusu namna ya kuendesha ushiriki wa sekta binafsi kwenye miradi ya nishati nchini.

"Kuna miradi inahitahi mtaji mkubwa kama vile Sh. trilioni mbili. Sekta binafsi wanapaswa kuungana na kufanya uwekezaji, serikali tuna uhusiano mzuri na sekta binafsi na kwamba wamekuwa msaada mkubwa hususani katika kutoa ajira pamoja na kutushauri katika masuala mbalimbali," alisema Makamba.

Alisema kwenye sekta ya nishati hususani utekelezaji wa miradi, serikali imekuwa ikiwatumia makandarasi wazawa.

Aidha, kwenye miradi mikubwa kama Mradi wa Gesi Asilia iliyosindikwa (LNG), serikali itaendelea kutegemea wawekezaji kutoka nje.

Alisisitiza azma ya serikali ya kuweka uwiano wa maendeleo ya nishati vijijini na mijini, kutaja vipaumbele kuwa ni pamoja na kuboresha ufanisi wa nishati na kuongeza utegemezi wa sekta hiyo.

Alihimiza ushiriki wa sekta binafsi katika mnyororo wa thamani wa nishati mbalimbali nchini.

Mwenyekiti wa CEOrt, David Tarimo, alisema sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi, na inashirikiana na serikali wakati wote.

Alisema katika nishati sekta binafsi inatoa mchango mkubwa katika kukuza uwekezaji na kujikita katika kuukuza na kuwa kipengele muhimu kwa kutegemea michango ya kimkakati na ushiriki katika kufungua fursa chipukizi nchini.

"Sekta binafsi tukipewa nafasi tunaweza, kwa sababu tumekuwa chachu katika ukuaji wa uchumi, miradi mingi hapa nchini inaendeshwa na sekta binafsi hali iliyochangia ukuaji wa uchumi na kuchochea mageuzi katika soko la ajira.




Mkurugenzi wa Rasilimaliwatu Vodacom Tanzania Plc, Vivienne Penessis (kulia), akizungumza na watoto wa wafanyakazi wa kampuni hiyo wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa masomo ya sayansi na teknolojia (STEM) iliyoambatana na kampeni ya 'Bring Your Child to Work' inayoendana na huduma za Vodacom, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni mtoa mafunzo hayo, Dk. Isaya Ipyana kutoka Taasisi ya Project Inspire. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi wakoshwa na TANROADS udhibiti ajali

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

WANANCHI wa Kata ya Buigiri, Wilaya Chamwino mkoani Dodoma wameupongeza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa kuwawekea matuta na alama za barabarani ili kudhibiti ajali za mara kwa mara zinazotokea eneo la Buigiri.

Wakizungumza na Nipashe jana wilayani hapo, wananchi hao walisema kwa takriban miaka minane wamekuwa wakishuhudia ajali za mara kwa mara kutokana na ukosefu wa matatu na alama za barabarani.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa Wilaya hiyo, Godwin Madeje, alisema: "Kwa kipindi kirefu tumekuwa tukiwapoteza wazee wenzetu wengi kupitia ajali za barabarani kutokana na kutokuwapo kwa alama za barabarani pamoja na matuta.

"Eneo letu la vijiji vitatu vya Buigiri, Chinangali na Mwegamile linapitiwa na barabara ya Dodoma-Morogoro inayotumiwa na magari mengi pamoja na mabasi yanayokwenda kwa kasi sana."

Mzee huyo alisema waathirika wakubwa wa ajali hizo ni wanafunzi, wazee, watu wenye ulemavu na watumiaji wengine wa barabara.

Mwalimu mstaafu, Michael Msuya, alisema ipo haja serikali kuhakikisha Jeshi la Polisi linaweka mifumo endelevu ya kusimamia madereva, hususan wale wanaoendesha magari ya mwendo kasi kwenye maeneo yenye alama zinazozuia mwendo kasi.

Mchungaji Julias Chigo wa Kanisa la Angalikana Buigiri, alisema hatua iliyochukuliwa na serikali ya kuweka matuta na alama za barabarani ni kuwajali wananchi wa kata hiyo ambao wamekuwa na kilio hicho kwa muda mrefu.

"Wananchi wa kata hii walikuwa wakigongwa kama wanyama, hivyo tunamshukuru Rais wetu kwa kusikia kilio chetu na tunaamini sasa vifo vitapungua hasa kwa makundi ya watoto, wasioona, na wenye ulemavu mwingine na wazee ambao walikuwa ni waathirika wa ajali hizo," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chamwino, Keneth Yindi, alisema kuwa tangu mwaka 2015, wananchi wa kata hiyo wamekuwa na kilio cha kuiomba serikali kuwekewa matuta na alama za barabarani.

Alisema kilio hicho ni kutokana na wananchi wa eneo hilo kukutwa na majanga ya kugongwa mara kwa mara na kusababisha vifo na ulemavu wa kudumu.

"Kuanzia mwaka 2016 nilikuwa ninakwenda mara kwa mara wizarani kuomba utatuzi wa suala hili kwenye kata yangu ambayo ipo kwenye barabara ya kutoka Dodoma kwenda Morogoro.

"Nilitaka waweke matuta ili kunusuru maisha ya wakazi hasa kwenye maeneo yaliyopo shule maalum ya wasioona, kambi ya walemavu wasioona ya matembe bora," alisema.

Aliwataka wananchi, pamoja na kuwekewa alama hizo, wazingatie matumizi bora ya barabara ili kutosababisha ajali.

# Serikali yalegeza masharti ujenzi vituo mafuta vijijini

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imetenga Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kusaidia wajasiriamali wanaotaka kuwekeza kwenye vituo vya mafuta ya petroli na dizeli katika maeneo ya vijijini ili kuwaondolea wananchi kero ya kukosa huduma hiyo.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake, Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), Kanda ya Ziwa, George Mhina, alisema fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo muhimu kwa maendeleo yao.

Alisema EWURA imepunguza masharti ya ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini na kwa sasa mjasiriamali anaweza kujenga kwa gharama ya Sh. milioni 40 hadi kukamilika.

Kadhalika, alisema vituo vya mafuta maeneo ya mijini ujenzi wake una masharti magumu yakiwamo ya kiwanja kuwa na hati pamoja na kituo kimoja kugharimu zaidi ya Sh. milioni 300.

Mhina alisema serikali imelegeza masharti ya ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo kwa gharama nafuu iliyopangwa na serikali.

Alisema kwa sasa wafanyabiashara wanaouza mafuta kwenye chupa za maji huko vijijini wanauza kwa bei wanayoitaka jambo ambalo linawaumiza wananchi.

"Serikali imepunguza masharti ya uanzishwaji wa vituo vya mafuta huko vijijini na imetenga fedha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyabiashara watakaotaka kufanya biashara hiyo, hii ni fursa kwa wanaotaka kufanya hivyo," alisema Mhina.

Alisema maeneo mengi katika Kanda ya Ziwa wananchi wanauza mafuta kiholela na mpango huo utasaidia kumalizia tatizo hilo kwa kuwa bidhaa hiyo itapatikana kirahisi vijijini.

Mhina alisema kupitia mpango huo mfanyabiashara anaweza kujenga na kufungua kituo cha mafuta hata kama kiwanja hakina hati na kinachotakiwa ni muhtasari wa mkutano wa kijiji ambacho kimempa eneo la kujenga.




Mkurugenzi Msaidizi wa Southern Tanzania Elephant (STEP), Frank Lihwa (kushoto), akimkabidhi Kamishna Msaidizi wa Utalii Kanda ya Kati, Adrehem Nziku (wa pili kulia), gari kwa ajili ya shughuli za uhifadhi kwenye mapori yaliyoko Kanda ya Kati. **PICHA: JUMBE ISMAILLY**

# Wakulima waelezwa umuhimu kuvuna karafuu zilizokomaa

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAKULIMA wa zao la karafuu kisiwani Pemba wametakiwa kuchuma karafuu zilizo komaa ili waweze kupata faida kubwa sokoni.

Waziri wa Biashara Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, alisema hayo wakati akizindua zoezi la uchumaji wa karafuu, Kichunjuu mkoani Pemba.

Alisema, endapo wakulima wa zao hilo watachuma karafuu zinazostahiki kuchumwa watapata faida kubwa kwao na serikali pia.

Waziri Shaaban alisema, kwa mwaka huu serikali imedhamiria kurudisha hadhi ya zao la karafuu ya Zanzibar kuwa na ubora wake kwa kuliimarisha kwa kuwa tayari Shirika limeshakaa na wadau mbalimbali wa zao hilo.

"Mashine ambazo tumeziweka katika vituo vyetu vya kununulia karafuu ziko salama na zimethibishwa na kuthibitika kwamba zina ubora na wala haziharibu karafuu kama inavyodaiwa," alisema Waziri Shaaban.

Pia katika suala zima la ubora wa karafuu, hili ni kutokana ushughulikiaji wake kuanzia inapochumwa, uanikaji wake, lakini hata matunzo yake, hii ndiyo njia itakayosaidia kupata karafuu mzuri," alisema.

Alisema, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua changamoto zote zilizomo kwenye kilimo cha karafuu, na inajadili changamoto hizo kuhakikisha inahuwisha kilimo hicho ili kiweze kurudi kama zama zilizopita.

Waziri Shaaban alisema kuwa, jitihada za ziada zinatakiwa kuchukuliwa ili mkulima aweze kumudu gharama za ushughulikiaji wa mashamba yao na kuweza kupanda miche yenye ubora na yenye kutoa mazao kwa wingi.

"Rais amekuwa akituongoza kwa hilo na tayari tunajadili ndani ya serikali mpango mkubwa wa kukuza kilimo cha karafuu na baada ya muda tutaona mabadiliko yake," alisema.

Aliwatahadharisha wananchi wote ambao wanajushughulisha na wizi wa kuwa karafuu na kusema kuwa, kwa sasa mwarobaini wa tatizo hilo umeshapatikana.

Alisema mwananchi yeyote ambaye atapatikana na hatia ya kuiba karafuu ikiwa ni majumbani au shambani kesi yake ni kuhujumu uchumi wa nchi.

"Kwa wale wanaojishughulisha na utoroshaji wa karafuu mbinu zao tumeshazijua, tutaendelea kushirikiana na vikosi vyetu vya ulinzi na usalama ili kuona vitendo hivyo vinadhibitiwa," alionya.

Naye mkulima Hafidh Makame Haji, kutoka Michenzani mkoani Pemba alisema, kwa mwaka huu mauzo ya karafuu ni tofauti na miaka iliyopita nyuma hasa katika sehemu ya kupasishia karafuu kutokana na uwekwaji wa mashine, ingawa wanaamini kuwa mashine hizo ziko salama.

## Wahitimu wa vyuo vikuu wapewa mbinu wajiajiri

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewataka wahitimu wa vyuo vikuu kuwa wabunifu na kuanzisha vitu vitakavyowawezesha kujiajiri na kujiingizia kipato badala ya kuwa na mawazo ya kusubiri kuajiriwa wanapohitimu.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, kwenye mahafali ya tatu ya wanafunzi waliosoma nje ya nchi yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Mgeni rasmi kwenye mahafali hayo yaliyoandaliwa na Global Education Link, alikuwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Juma Kipanga na wageni wengine ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini na mabalozi mbalimbali wanaoziwakilisha nchi zao.

Dk. Mollel alisema badala ya kuendeleza kasumba ya kutembea na vyeti kutafuta ajira, wahitimu hao wanaweza kubuni vitu vitakavyowazalishia fedha nyingi na kuajiri wenzao wenye taaluma mbalimbali.

"Kwani hamjaona mtu wa darasa la saba ameanzisha kampuni akamwajiri Profesa? Kuna watu wamesoma hadi ngazi ya kuwa Profesa, lakini ukimwondoa kwenye ajira hana lolote lile kwa hiyo msiwe kama hao, nyinyi muwe wabunifu mjiajiri na kuajiri na wengine," alisisitiza Dk. Mollel.

Pia, aliiagiza Taasisi ya Global Education Link (GEL) kumpelekea kero zinazowakabili wahitimu wa vyuo vikuu nje ya nchi ili azifanyie kazi na wataalamu wake kuwapunguzia mzigo wazazi.

Alitoa agizo hilo kutokana na kero mbalimbali zilizotolewa na Mkurugenzi wa GEL, Abdulmalik Mollel kwenye mahafali hayo.

"Mollel umetaja changamoto nyingi sana sasa naomba niandikie niletee wizarani nitaitisha kikao na wataalamu wangu tutatue changamoto moja baada ya nyingine ili tuwasaidie wazazi ambao wametumia muda na rasilimali zao kuwasomesha," alisema Dk. Mollel.

Alisema serikali imewekeza kiasi kikubwa kwenye sekta ya afya zikiwano Sh. trilioni 1.3 zilizotolewa kupambana na UVIKO-19 na wataalamu hao wanahitajika kwenye maeneo mengi nchini.

Alitaka wahitimu hao watembezwe kwenye Taasisi ya Moyo ya (JKCI), Muhimbili na Mloganzila kuona uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali ili wasiwe na ndoto za kufanyakazi nje ya nchi.

"Kuthibitisha hilo juzi Waziri wa Afya wa Malawi alikuja nchini akatembelea JKCI kuangalia uwekezaji tulioufanya alishangaa mambo makubwa na tumekubaliana walete wagonjwa wao hapa badala ya kuwapeleka Ulaya na India," alisema Dk. Mollel.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini, aliipongeza GEL na Mkurugenzi wake kwa wanavyofuatilia maendeleo ya wanafunzi nje ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa GEL, Mollel alisema asilimia 50 ya wahitimu hao wamesomea fani ya afya ikiwamo udaktari na ufamasia.

Aliomba serikali itoe mikopo kwa wanafunzi wanaosoma nje ya nchi kwa kuwa nao watakuja kuijenga nchi wanapohitimu masomo yao.

Alisema wazazi wengi wanaosomesha watoto wao nje ya nchi hawana kipato kikubwa wanajibana na kuachana na mambo mengine ili kufanikisha elimu kwa watoto wao.

Alisema wahitimu hao wameiva vya kutosha kufanyakazi eneo lolote na aliwaomba waajiri ikiwamo serikali kuwachukua kwenye nafasi hizo.

"Mheshimiwa Waziri nikuhakikishie hawa wahitimu ni bora na wamehitimu kutoka vyuo bora kabisa duniani wajaribu kwa kuwachukua na kuwapa nafasi mbalimbali mtaona kazi kubwa watakayofanya," alisema Mollel.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 23, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



## Msaada kisheria unavyoinua haki za wanyonge na kinamama vijijini

Ukurasa 13



Ukurasa 12

## Wenye ulemavu hawa wana jambo lao elimu ya kidigitali

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBITI

# Kilimo kinavyowaathiri mabinti Kibiti, chaweka mazingira ya mimba utotoni

## ■100 waanguka sekondari, msingi miaka 2

KUNA usemi kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa taifa, kuwa ndicho kinachozalisha chakula kutoka kwenye mazao na mifugo tena ni chanzo cha malighafi za viwanda vingi.

Lakini, wapo baadhi wanaoweza kukilaani kuwa kimekuwa chanzo cha kubadilika na kuharibika maisha yao, hawa ni wasichana kwa sababu wapo waliobakwa wakilinda (kuamia) mazao shambani au wakilisha mifugo porini. Zote ni kazi za kilimo.

Kwa wanafunzi wa Halmashauri ya Kibiti Mkoa wa Pwani, kimekuwa uti wa mgongo wa mimba za wanafunzi na mabinti vijijini, kwa sababu walezi na wazazi wanapokwenda mashambani na kuwaacha watoto peke yao nyumbani 'waharibifu' hutumia mwanya huo kuwaghilibu na kuwaacha wajawazito.

Inaelezwa kuwa wakulima hao hukaa mashambani na kurejea baada ya miezi sita na hapo wasichana wengi wanadanganywa na kupewa mimba na kuacha shule.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kibiti Mohamed Mavula, anaeleza kuwa ongezeko la mimba ni kitishio kinachozuia wasichana kupata elimu.

Anataja takwimu zinazoonyesha kuwa shule za msingi na sekondari kote wanaathirika, mwaka 2020 wanafunzi 22 walikatisha masomo kwa mimba, mwaka jana walikuwa 36 na kuanzia Januari hadi Juni mwaka 2022 wasichana 32 wamekatishwa masomo pia.



Wasichana wana haki ya kulindwa ili wasome na kumudu maisha yao. **PICHA: MTANDAO**

Anaeleza kuwa ongezeko la mimba linachangiwa na watoto kuishi wenyewe wazazi na walezi wao wakiwa mashambani maeneo ya Delta na Rufiji.

"Ni kawaida kuwaacha watoto wenyewe watu wazima wakiwa kwenye shughuli za kilimo, tumeendelea kutoa elimu kwa wazazi kwa kushirikiana kamati za ulinzi za wilaya, kata na kwenye vijiji, vitongoji waweze kuweka taratibu za namna watoto watakaishi kipindi cha kilimo," anasema.

Mkurugenzi anasema wanaopata mimba walio wengi wamekuwa kikwazo kutoa ushirikiano wa kuwakamata wanaohusika.

"Mimba ambazo tumekuwa tukizigundua kuanzia ngazi ya kijiji zinaripotiwa kwa watendaji lakini kesi ikifika polisi wazazi na walezi hawaendi kutoa ushahidi na watoto wenye ujauzito wanakwamisha kwa kudai wamepata mimba kwenye mazingira ambayo hayana ushahidi," anasema Mavula.

"Tumeendelea kutoa elimu kwa watoto hasa wa kike namna gani waendelee kuheshimu masomo na kujiheshimu ili kujiepusha na mambo yanayoweza kukatisha masomo yao," anaongeza.

Anasema wamegundua kuwa minada nayo inasababisha kupata mimba na kwamba wamekuwa wakitoa elimu kwa wazazi, walezi, jamii na wengine kusaidia kuokoa watoto kwa kuzuia wenye umri wa kwenda shule waende darasani siyo kutumwa kwenye minada, ili kuwaepushia vishawishi.

Mkurugenzi huyo anasema anaamini endapo wazazi, walezi na viongozi kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji na kata wakishirikiana ipasavyo kutekeleza mikakati hiyo watakomeza vitendo vya mimba shuleni.

Diwani wa Mtwanya Wilaya ya Kibiti Malela Toka, anaeleza kuwa katika kipindi hicho cha miezi sita wanafunzi 11 katika kata hiyo wamekatisha masomo kwa mimba.

Malela anasema mazingira ya baadhi ya familia kutowajibika ipasavyo pamoja na hali duni za maisha ni miongoni mwa sababu za ongezeko la mimba.

Aidha, diwani huyo anaeleza kuwa ushirikiano mdogo wa wazazi na walezi ambao watoto wao wamepata mimba ili kuwachukulia hatua watuhumiwa ni sababu za wengine kuendelea kuwapa ujauzito wanafunzi hao.

Anasema elimu kwa wazazi na walezi inaendelea kutolewa ili kupunguza idadi ya wanafunzi wanaokatishwa masomo kwa mimba na kuwahimiza wawe wafuatiliaji na kusimamia, kuchukua hatua kwa wahusika badala ya kushirikiana nao.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kinyanya Kati kwenye halmashauri hiyo, Abdallah Tindwa, anasema wanafunzi wengi wa kike kuishi peke yao nyumbani ni moja ya sababu za kuangukia kupata mimba.

Anasema amekuwa akiwaita baadhi ya wazazi na kuongea nao anapobaini mienendo ya tabia ya watoto wao lakini hakujawa na mabadiliko.

Lakini mwenyekiti huyo anawageuzia pia kibao baadhi ya madereva bodaboda ambao wanawapatia lifti wanafunzi wasio na nauli ya kuwafikisha shule asubuhi na jioni wanaporudi nyumbani.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Wenye ulemavu hawa wana jambo lao elimu ya kidigitali



Mtaalamu wa lugha ya alama akiwatafsiria wasiosikia, katika kongamano la maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani, lililofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: SABATO KASIKA**

TEKNOLOJIA katika elimu ni jambo lisilokwepeka hasa kwenye dunia inayozidi kuwa ya kidigitali inayobadilisha kwa haraka namna watu wanavyoishi.

Maendeleo ya teknolojia katika jamii yamesababisha mahitaji ya ujuzi wa msingi katika mifumo ya elimu, na hiyo ndiyo sababu taasisi kuanzia shule za msingi hadi vyuo vya kati na vya juu kurekebisha mitaala ya 'kizamani' ili iendane na masuala ya kidijitali, hilo nalo sasa likihitajika kwa wenye mahitaji maalumu.

Anasema Janeth Lugome, ambaye hasikii na kiongozi wa jukwaa la Global Platform, anayeomba elimu kwa wanafunzi viziwi iwe ni ya kidigitali.

Aliyasema, hayo wiki iliyopita kwenye kongamano la Siku ya Vijana Duniani, jijini Dar es Salaam, inayoadhimishwa Agosti 12 kila mwaka.

Anabainisha kuwa miundombinu ya kufundishia si rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu wakiwamo viziwi.

"Linapokuja suala la kujifunza kwa kutumia picha, wasiosikia zinatumika za kuchora au zilizoandaliwa wakati wa kufundishwa na hubandikiwa ukutani, ninadhani ipo haja wafundishwe kidigitali," anasema Janeth.

Anafafanua kuwa, anatamani zitumike picha za video zinazoonyesha uhalisia badala ya kutumia za kuchora ambazo wakati mwingine inakuwa vigumu kuelezea kwa ufasaha.

Anasema iwapo hilo litafanyika, itakuwa rahisi kwa wanafunzi hao kuelewa kile wanachofundishwa, kwa maelezo kuwa bila kutumia njia hiyo wataendelea kubaki nyuma wakati dunia inazidi kwenda mbele.

Janeth, anazungumzia umuhimu wa elimu jumuishi, akisema ina faida ikiwa ni pamoja na kuleta usawa kwa watoto wote, kutoa fura sawa za ujifunzaji, kupunguza utegemezi katika jamii, kuwapunguzia gharama wazazi, kuwatia moyo wenye ulemavu na mahitaji maalumu ili kuleta maendeleo ya kielimu katika familia na taifa.

"Elimu jumuishi inalenga kufuta ujinga na umaskini kwa watu wote bila ya kujali hali zao, kwani utekelezaji wa elimu jumuishi darasani ni kuhakikisha kuwa hakuna mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu anayeachwa nyuma," anasema.

Kujifunza huko kunajumuisha kila mtoto au mtu kwa ngazi zote ikiwaweka pamoja wasio na ulemavu na wenye ulemavu na walio na mahitaji maalum ya elimu, wote wakijifunza pamoja katika shule za msingi, sekondari, vyuoni na vyuo vya elimu ya juu.

**TUTAZAMWE WOTE**

Zaidi, Janeth ana jambo lake kwa serikali:"Lakini nina ombi lingine ambalo linahusu uteuzi wa nafasi mbalimbali za uongozi. Hakuna uwiano, kwani wanaopewa nafasi kubwa ni wanaoishi na ualbino, wasioona, na wasiosikia wamesahaulika."

Kiongozi wa Global Platform, anasema sauti ya wasiosikia, bado haijasikiwa wala kuitikiwa hivyo, anaomba kila kundi la watu wenye ulemavu lipewe nafasi katika uteuzi kuanzia ngazi ya chini hadi juu, kwa kuwa wana mchango katika maendeleo ya taifa.

Mratibu wa Programu wa Youth Forum, Evalyn Mwambungu, anasema vijana hasa wa kike wanahitaji kushikwa mkono ili kufikia usawa wa kijinsia katika uongozi, kwa kuwa bila kufanya hivyo hawawezi kufika mbali.

"Maana yangu ni kwamba wawezeshwe kupata elimu na pia kuteuliwa kwenye nafasi mbalimbali, kwani ingawa wapo waliotеuliwa, bado idadi hiyo inatakiwa kuongezeka zaidi," anasema Evalyn.

Kadhalika, anawataka wasichana na vijana wengine kutiana moyo, ili wasome kwa bidii na kukwepa vikwazo mbalimbali ikiwamo rushwa ya ngono inayokwamisha kufikia ndoto zao.

> "Pamoja na hayo, Kitengo cha Huduma za ajira (TaESA), kinatakiwa kuwafuata vijana katika taasisi za elimu na kuwaelezea fursa za ajira na namna ya kukabiliana na soko la ajira hasa wale wanaokaribia kuhitimu masomo yao kwa kuwapa mafunzo maalumu ya kuwajengeaa kujiamini, namna ya kuandaa wasifu wao pamoja na namna ya kukabiliana na waajiri wao," anasema.

"Hilo likifanyika, vijana wa kike wataendelea kuongezeka katika vyuo nchini na hata kuongezeka kwenye uteuzi wa ngazi mbalimbali za uongozi na hivyo kuleta usawa wa kijinsia katika nafasi hizo," anasema.

**MAFUNZO YA KUJIAMINI**

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, anawataka vijana wanaohitimu kwenye vyuo mbalimbali nchini kuchangamkia fursa ya mafunzo yanayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi.

Anasema, ofisi hiyo ina Kitengo cha Huduma za Ajira (TaESA), kwa ajili ya kuwajenga vijana kuwa na mtazamo chanya ambao umewasaidia kujiamini kazini.

"Kutokana na kazi ambazo zinatolewa kuwa na uhitaji wa mtu mwenye uzoefu, serikali imekuja na mfumo huo wa mafunzo ya vitendo mahali pa kazi, kuwajengea vijana uzoefu na kukuza uelewa wao," anasema Katambi.

Anafafanua kuwa, mafunzo hayo yanahusu wanafunzi wote wakiwamo wenye ulemavu wa aina mbalimbali na kwamba ni muhimu kila aliyehitimu akajitokeza kupata mbinu za kukabiliana na ukosefu wa ajira.

Katambi, anasema serikali imeendelea kutengeneza mazingira wezeshi na kuongeza fursa za ajira kwa vijana kupitia miradi mbalimbali ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa.

"Pamoja na hayo, Kitengo cha Huduma za ajira (TaESA), kinatakiwa kuwafuata vijana katika taasisi za elimu na kuwaelezea fursa za ajira na namna ya kukabiliana na soko la ajira hasa wale wanaokaribia kuhitimu masomo yao kwa kuwapa mafunzo maalumu ya kuwajengeaa kujiamini, namna ya kuandaa wasifu wao pamoja na namna ya kukabiliana na waajiri wao," anasema.

Januari mwaka huu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilizindua Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa miaka mitano utakaohitimishwa mwaka 2026 wenye lengo la kutoa elimu kwa wote pamoja na makundi yenye mahitaji maalumu.

Akizindua mkakati huo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Eliamani Sedoyeka, anasema utawajumuisha makundi yote maalumu kuanzia ngazi ya awali hadi elimu ya juu na kwamba, utatoa dira ya maendeleo kielimu na utasaidia upatikanaji wa wanafunzi wa awali na wale ambao hawajaanza shule.

ELIMU

NA SALOME KITOMARI

# Msaada kisheria unavyoinua haki za wanyonge na kinamama vijijini




Wanakijiji cha Nyakadete kilichoko Mbeya, wakijifunza masuala ya haki na huduma za msaada wa kisheria. **PICHA: MWANDISHI WETU**

SERIKALI ina wajibu wa kuhakikisha upatikanaji wa haki sawa. Jukumu hilo linajumuisha utoaji wa msaada wa kisheria bila malipo kwa Watanzania ambao hawana njia au uwezo wa kulipia huduma hiyo.

Kwa kufahamu kuwa kukosekana kwa msaada wa kisheria bila malipo ni kikwazo cha upatikanaji sawa wa haki, unaoathiri makundi yasiyo na uwezo, serikali ilitunga sheria ya msaada wa kisheria mwaka 2017, kwa ajili ya kuruhusu ambao hawana uwezo wasaidiwe kupata haki mahakamani.

Kuwapo kwa sheria na kanuni zake kupatikana mwaka 2018, kumeweka taratibu za kutoa huduma hiyo muhimu zinazowahakikishia wananchi usawa na haki mbele ya sheria.

Utekelezaji wa sheria ya msaada wa kisheria, umekuwa wa mafanikio na kuwahakikishia wananchi upatikanaji wa haki kwa wakati, hasa kwa wanawake na watoto wanaoishi vijijini na maeneo ambayo ingekuwa vigumu kupata haki. Mtandao wa mashirika yanayotoa huduma ya msaada wa kisheria (TANLAP), kwa kushirikiana na Shirika la USAID la Marekani wanaendesha mradi wa mwanamke imara katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Kilimanjaro, unaoelezwa na Mkurugenzi wa TANLAP, Christina Kamili, kuwa umenufaisha wananchi.

Anasema, umewawezesha kupata huduma ya msaada wa kisheria kwenye masuala mbalimbali ya haki.

Aidha, chini ya mradi huo wametoa mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria 95, na sasa ni chachu ya



Mkurugenzi wa TANLAP Christina Kamili.

kufanikisha upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi kwenye maeneo ya mradi, Mkurugenzi wa TANLAP anabainisha.

Aidha, matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa sheria hiyo unaofanywa na TANLAP pamoja na Chama cha Wanawake Wanasheria (TAWLA), WiLDAF na KWIECO kwenye mradi wa mwanamke imara unaonyesha kuwa yapo mafanikio ya kupata na kutoa huduma ya msaada wa kisheria tangu kutungwa kwa sheria hiyo.

Mafanikio ni pamoja na sheria kuleta uratibu mzuri wa utoaji msaada wa kisheria kwa kuanzisha ofisi ya msajili wa watoa huduma ya msaada wa kisheria, kwenye Wizara ya Katiba na Sheria. Hii ni kwa sababu, awali taasisi zilizokuwa zikitoa msaada wa kisheria zilijiratibu zenyewe bila kuwapo chombo maalumu cha uratibu, anasema Christina.

Kadhalika, imeweka bodi ya kitaifa ya ushauri ya msaada wa kisheria ambayo inajumuisha watoa huduma, wasaidizi wa kisheria, pamoja na wadau wengine kutoka taasisi za serikali.

"Kuwapo kwa rejista maalumu kwa watoa huduma wa msaada wa kisheria na bodi ni muhimu kwa taifa na huduma ya msaada wa kisheria ni haki ya raia kama zilivyo nyingine. Ili kuleta usawa kufikia haki, asiye na uwezo wa kumudu gharama za mawakili anapata uwakilishi mahakamani kama ambaye anayeweza kumlipa wakili akamwakilisha kortini," anaeleza.

Aidha, anataja jambo muhimu, akisema sheria imetamka makundi yanayopata huduma ya msaada wa kisheria kuwa ni wasio na uwezo, maskini na makundi maalumu na imetamka kuwa mtoto ni lazima apate huduma kutoka kwa watoa huduma kwa mujibu wa sheria.

Mkurugenzi wa TANLAP, anaongeza kuwa sheria imewatambua wasaidizi wa kisheria ambao wamefuzu mafunzo maalumu ili watoe huduma kwa wananchi.

Anasema, uwepo wa wasaidizi hao umeongeza upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria vijijini ikiwa ni pamoja na maeneo unapotekelezwa mradi wa mwanamke imara.

Anasema: "Mradi unalenga kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wakati, kupinga na kuzuia ukatili wa kijinsia kwa wanawake na vijana, kuwahamasisha kushiriki nafasi za uongozi na vyombo vya maamuzi na pia kuwainua wanawake na vijana kiuchumi."

Pia, sheria imetafsiri ni nani msaidizi wa kisheria, mwanasheria na wakili katika kusaidia wananchi na imebainisha mipaka na majukumu yao, anasema.

Kwa sasa, wasaidizi wa kisheria, wanasheria na mawakili wanashirikiana katika kazi kwa mujibu wa sheria tofauti na ilivyokuwa kabla ya ujio wa sheria, baadhi ya wasaidizi walijitambulisha kuwa wanasheria. Sasa wanapewa vyeti vya utambulisho na wanazingatia mipaka yao.

"Lengo ni kufikia Tanzania yenye mwanamke imara anayepata haki kwa wakati, anayeshirikishwa kwenye uongozi, uchumi na isiyo na ukatili wa kijinsia," anafafanua.

**CHANGOMATO**

Christina anazitaja changamoto kadhaa za utekelezaji wa sheria ya huduma ya msaada wa kisheria, akigusia ada za usajili kwa wasaidizi wa kisheria na watoa huduma ya msaada wa kisheria, akisema ilikuwa kikwazo ilipunguza idadi ya wahudumu hao kwani walioshindwa kuzilipia.

Anapongeza hatia ya serikali kuifuta na kushauri yafanyike marekebisho kwenye sheria na kanuni ili kuwawezsha kufanyakazi kwa ufanisi.

Adha, anasema sheria haikuweka utaratibu wa kugharamia huduma ya msaada wa kisheria kama zilivyo nyingine na kwamba uzoefu kutoka mataifa mengine kama Kenya, unafundisha kuwa serikali inatenga kibajeti kwa ajili ya watoa huduma ya msaada wa kisheria.

"Kwa Tanzania jukumu limeachwa kwa mashirika na wasaidizi wa kisheria wanaotegemea wahisani ili kutoa msaada. Kukosekana fedha kunafifisha utoaji wa msaada hasa maeneo ya pembezoni,"anasema Christina.

Anautaja uhaba wa wasaidizi hao umefifisha upatikanaji wa huduma hiyo, na ili kuongeza idadi yao ni muhimu sheria na kanuni kuweka mpango endelevu wa jinsi ya kupata wapya ili kukidhi mahitaji.

Kadhalika, anataja tatizo la ukosefu wa ofisi na kwamba katika ngazi ya kata na vijiji hawana ofisi hivyo kushindwa kutoa huduma kikamilifu akishauri kuweka utaratibu wa kuwawekea ofisi kwenye kata ili kuboresha utoaji wa huduma hiyo.

**IJE SHERIA MPYA**

Christina anasema: "Taifa lenye utulivu ni muhimu kwa watu kujiletea maendeleo. Bado safari ni ndefu kufikia hatua hiyo kutokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia. Ndiyo maana tunataka bunge litunge sheria mahususi ya kupinga ukatili wa kijinsia ambayo itagusa kila kitu kuliko ilivyo sasa."

Mkurugenzi wa TANLAP, anasema kuna nyingi mfano ya mwenendo wa makosa ya jinai, ipo ya za kazi na sheria ya mtoto na nyingine nyingi ambazo zimeanisha makosa ya ukatili wa kijinsia na adhabu zake ambazo wakati mwingine huleta mkanganyiko.

"Hii ni moja ya sababu ya kuhitaji sheria mahusus ya kupinga ukatili wa kijinsia nchini ambayo itasimama yenyewe kama zilivyo nyingine mfano Sheria ya Kazi na Sheria ya Mtoto," anasema Christina.

Aidha, anasema kwa kupitia mradi wa Mwanamke Imara, TANLAP na watekelezaji wengine wameaanda rasimu mfano ya sheria ya kupinga ukatili wa kijinsia sambamba na kuanzisha Mtandao wa Masuala ya Kisheria ya Kifamilia, ili kutoa mchango na msukumo kupunguza mabyo yanayoleta ukatili.

Mkurugenzi anasema sheria hiyo ni muhimu kwani makosa na ukatili mwingi unaanzia kwenye mirathi kwa mwanamke kubaguliwa, wakitoka wanaingia kwenye ardhi ambaye ni rasilimali muhimu na baadaye jinai na wakati mwingine huishia kwenye mauaji.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Moshi; kitanzi cha jikoni kinachogharimu mamilioni

RIPOTI ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya 2019 ya athari za moshi wa kuni kwa binadamu, inaeleza kuwa takriban watu bilioni 2.8 wanazitegemea kupikia, licha ya kuwa chanzo cha magonjwa na vifo kwa mamilioni.

Mataifa yanayoendelea ndiyo yanayotumia kuni kwa asilimia 90, wakati asilimia 70 ya kaya zinazotumia kuni na mkaa zinaishi Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara ikiwamo Tanzania.

Moto wa kuni kavu iwe ndani au nje hutoa moshi na chembe ambazo zina athari mbaya kwa afya ya watumiaji, wawe wapishi jikoni, wanaoota moto na hata wale wanaoishi kwenye mazingira ambayo kuni hizo zinatumika.

Kuni ni chanzo cha nishati kinachochafua na kuharibu misitu na mapori tena ni hatari zaidi zama hizi za mabadiliko ya tabianchi.

Samadi, mkaa pamoja na kuni vinapotumiwa kupika ni kitisho kwa mazingira, binadamu na wanyama, kutokana na kutoa moshi wenye sumu.

Pamoja na kutumia kuni kuna mataifa ya Kusini ya Sahara yanayotegemea mafuta ya taa na vifaa vingine chafuzi kuangaza makazi yao usiku.

Athari za kiafya za nishati hii ni mbaya na kinamama ndiyo waathirikaji kwani huvuta moshi mzito kwa saa nyingi wanapotayarishia chakula, familia zao na huwasha moto ili kupasha joto nyumba wakati wa baridi hasa kipupwe na mvua.

**MAGONJWA HATARISHI**

WHO, inasema watoto, wazee, na watu wengine walio katika mazingira magumu wanateseka, wanawake wanaovuta moshi muda mwingi nyumbani wakati wa kuandaa vyakula wanaumia zaidi kuliko wengine.

> Utafiti mwingine unaonyesha kuwa mafuta ya taa yanayotumiwa kupikia nayo ni chanzo cha vifo katika umri mchanga ikikadiriwa kuwa watu milioni 4.3 hupoteza maisha kila mwaka.

Aidha, mwaka 2012, zaidi ya asilimia 60 ya vifo vyote vya umri mdogo vilitokana na uchafuzi wa hewa miongoni mwa wanawake na watoto.

Uchafuzi wa hewa ya kaya ni sababu muhimu ya hatari kwa afya ya mazingira duniani kote.

Utafiti mwingine unaonyesha kuwa mafuta ya taa yanayotumiwa kupikia nayo ni chanzo cha vifo katika umri mchanga ikikadiriwa kuwa watu milioni 4.3 hupoteza maisha kila mwaka.

Kati ya vifo hivyo, milioni 4.3, milioni 3.8 hutokana na magonjwa yasiyoambukiza ikikadiriwa kuwa asilimia 25 ya vifo vya kiharusi, asilimia 15 ni magonjwa ya moyo 'ischemic' wakati asilimia 17 ya vifo sababu ni saratani ya mapafu na zaidi ya asilimia 33 ya vifo vyote vilitokana na kuathirika mapafu.

Moshi unasababisha pia ugonjwa wa mtoto wa jicho na kuleta upofu kwa mataifa maskini.

Asilimia 60 ya vifo vyote vya umri mdogo, vinahusishwa na uchafuzi wa hewa kutokana na matumizi ya kuni majumbani na mitaani.

Moshi huo chanzo ni 'nimonia' muuaji mkubwa zaidi wa watoto wenye umri chini ya miaka mitano duniani kote zaidi katika nchi maskini.

Ugonjwa huu pia hupunguza maisha ya vijana karibu milioni kila mwaka. Tena zaidi ya asilimia 50 ya nimonia hizo hutokana na moshi unaotumika nyumbani, sehemu za huduma kama shuleni na hotelini.



Kupikia kuni zinazozalisha moshi hakumuachi mtu salama. Ni sababu kuu ya nimonia, mtoto wa jicho , saratani mapafuni na maradhi ya moyo. **PICHA: MAKTABA.**

## WANENAVYO MALENGA

# TAFUTA WAKOSOAJI

TAFUTA wakosoaji, wale wanahojihoji,
Ambao wana kipaji, kile unakihitaji,
Tafuta hata kilaji, wakupe yasofariji,
Hivyo ulivyo hutoshi, sifa zinakukausha.

Hao washangiliaji, nasema huwahitaji,
Kwako wataka soseji, ulishe hata kijiji,
Wanaleta ujuaji, wakuloweshe na maji,
Hivyo ulivyo hutoshi, sifa zinakukausha.

Wakosoaji mtaji, pesa hawazihitaji,
Ukijiona hawaji, jishushe wawe mtaji,
Kesho upige buruji, ukishakuza kipaji,
Hivyo ulivyo hutoshi, sifa zinakukausha.

Ukishajiona gwiji, wa kujivika mataji,
Wenye hoja wahitaji, kwako ni wasumbuaji,
Wakushushe ujihoji, utasema huhitaji,
Hivyo ulivyo hutoshi, sifa zinakukausha.

Hao washangiliaji, wapo wengi kama jiji,
Kama bwawa wewe maji, wao waogeleaji,
Wanakufanya friji, wanywe ya baridi maji,
Hivyo ulivyo hutoshi, sifa zinakukausha.

Yao ya kukufariji, uwaone washikaji,
Usijedhani majaji, ni mbovu yao hojaji,
Wana yao mahitaji, kwa wazi hawayataji,
Hivyo ulivyo hutoshi, sifa zinakukausha.

Wajua una kipaji, kinachotoa mapaji,
Ni mafuta ya kufoji, wakudanganye huchuji,
Kwako wazidi kuhiji, kibidi uwe ni loji,
Hivyo ulivyo hutoshi, sifa zinakukausha.

Wakupigia buruji, ujione hauvuji,
Haki siyo hauvuji, wafaa kuvikwa taji,
Kwako wapata ulaji, vipi wakuhojihoji?
Hivyo ulivyo hutoshi, sifa zinakukausha.

Hao wengi wapitaji, tena wapenda kilaji,
Kama ndululu haziji, sifa zako hawataji,
Kusikia sitaraji, imekwishashuka geji,
Hivyo ulivyo hutoshi, sifa zinakukausha.

Pengine bora taraji, upate wakosoaji,
Wakubane wakuhoji, akili zako zichaji,
Hao unawahitaji, siyo washangiliaji,
Hivyo ulivyo hutoshi, sifa zinakukausha.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**





# Wananchi kupiga simu bila malipo kutoa taarifa sensa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI Watanzania wakihesabiwa leo katika siku ya sensa kitaifa, uongozi wa Mkoa wa Dodoma umezindua namba maalum ya simu ambayo kaya yoyote isipofikiwa na karani kuhesabiwa, mwananchi atapiga bila malipo kutoa taarifa.

Mkuu Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akizungumzia utaratibu huo jana jijini hapo, alisema lengo ni kuhakikisha watu wanahesabiwa.

"Mwananchi atapiga simu kupitia namba za bure ambazo ni 0800110083 na kueleza mtaa au kitongoji anapoishi na uongozi wa mkoa utawasiliana na karani aliyepangiwa katika eneo hilo na kufika kuhesabu kaya husika," alisema.

Mkuu wa Mkoa alisema maandalizi ya sensa yamekamilika ikiwamo mafunzo kwa makarani, vifaa vya sensa, usafiri na masuala ya kifedha kwa ajili ya kuwezesha sensa kufanyika.

"Hadi sasa makarani wamesambaa katika maeneo yao waliyopangiwa kwa ajili ya kujitambulisha kwa viongozi wa maeneo hayo na kutambua eneo lake la kuhesabu watu katika eneo lake ambapo Mkoa wa Dodoma una jumla ya makarani 10,353 ambao watafanya kazi ya kuhesabu katika maeneo waliyopangiwa.

"Serikali inawaomba wananchi wote kushiriki sensa kuanzia siku ya Jumanne (leo), mnatakiwa kutambua kuwa ni kosa kisheria kukataa kushiriki," alionya.

Pia aliwataka wananchi kuandaa taarifa za kaya ili kurahisisha kazi hiyo ikiwamo umri wa wanakaya, hali ya ajira, elimu, taarifa za kilimo na mifugo, namba za kitambulisho cha taifa (NIDA) na namba ya simu ya wanakaya.

"Makarani hakikisheni watu wanahesabiwa ipasavyo na kwa ufasaha na kutunza siri za kaya ulizohoji na kutambua kazi hiyo inafanyika kwa maslahi ya taifa katika kupanga mipango ya maendeleo.

"Nitumie fursa hii kuwasisitiza wakuu wa wilaya zote wa Mkoa wa Dodoma kwa kushirikiana na kamati za ulinzi na usalama za wilaya na wakurugenzi wa halmashauri, kuhakikisha wanasimamia zoezi hilo ili lifanyike kwa mafanikio kama ilivyopangwa," aliagiza.

## Chuo cha Mipango kuongeza udahili

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

CHUO cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) kipo kwenye hatua za mwisho kukamilisha ujenzi wa mradi wa upanuzi wa miundombinu ya mafunzo na malazi ili kuongeza wigo wa udahili wa wanafunzi.

Mradi huo unahusisha ujenzi wa hosteli mpya nne za kisasa, kila moja ikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wasiopungua 192 na miundombinu ya mafunzo, ikiwa ni pamoja na ukumbi wa kisasa wa mihadhara na madarasa.

Naibu Mkuu wa Chuo (Taaluma, Utafiti na Ushauri), Prof. Provident Dimoso, akizungumza na Nipashe jana jijini hapo, alisema mradi huo unalenga kuboresha utoaji wa mafunzo.

"Tunatekeleza mradi huu ili kutuwezesha kutoa elimu bora, kimsingi tukiwa na lengo adhimu la kuwapa wanafunzi maarifa na ujuzi wa kushindana kikamilifu katika soko la ajira, lakini kujiajiri wenyewe katika miradi mbalimbali ya kujikwamua kiuchumi," alisema.

Prof. Dimoso alisema hadi sasa chuo kina hekta 700 kwa ajili ya mradi huo wa upanuzi wa miundombinu katika tawi lake la Dodoma huku tawi lake la Mwanza wamenunua hekta 80 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

"Tunashukuru na kuthamini msaada mkubwa tunaoupata kutoka kwa serikali ambao umetuwezesha kutekeleza mradi huu na mingine mingi," alisema.

Aliongeza kuwa chuo hicho pia kinatekeleza mpango mkakati wa kutafiti na kuandaa mitaala ya kufundishia ambao unalenga kutoa majibu ya mahitaji ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi yanayohitajika nchini.

Chuo hicho kimeanzishwa na serikali kwa lengo la kuwandaa wataalamu wa kuchochea maendeleo ya kiuchumi kuanzia ngazi za vijijini.



Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Dodoma, Mariamu Ditopile, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) jijini Dodoma jana, pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa ruzuku aliyoitoa kwenye mbolea na kumwomba akutane na kundi hilo ili watoe kero zao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge ampongeza Rais Samia mageuzi ya kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma, Mariam Ditopile, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa Sh. bilioni 150 ruzuku ya mbolea kwa ajili ya kupunguza makali ya bei ya bidhaa hiyo nchini.

Aidha, alimwomba Rais Samia akutane na wakulima wadogo, wakubwa, wawekezaji na wadau wa sekta ya kilimo ili kusikiliza ushauri na maoni yao.

Aliyasema hayo jana jijini hapo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu serikali ilivyoleta mageuzi makubwa kwenye sekta ya kilimo kwa kuongeza bajeti na kumpongeza Rais Samia kwa jambo la kihistoria la ugawaji ruzuku ya mbolea.

Alibainisha kuwa kwa sasa matumizi ya mbolea nchini yanakadiriwa kuwa kilo 19 na virutubisho kwa hekta na kwamba kiasi hicho cha matumizi ni kidogo ikilinganishwa na nchi nyingine zilizopo chini ya Jangwa la Sahara na Afrika Kusini inatumia takribani kilo 58.5 za virutubisho kwa hekta.

"Matumizi madogo ya mbolea yamekuwa yakiathiri uzalishaji na tija kwa mfano kwa zao la mahindi wastani wa uzalishaji ni tani 1.45 kwa hekta, wakati tafiti zinaonyesha nchi nyingine kama Misri ambazo zinatumia mbolea kwa wingi na kwa usahihi zinazalisha hadi kufikia tani nane za mahindi kwa hekta," alisema.

Alifafanua kuwa matumizi madogo ya mbolea nchini yanasababishwa na gharama kubwa za mbolea na uelewa mdogo wa wakulima na kutakuwa na masoko ya uhakika ya mazao.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni 150 kama ruzuku ili kwenda kupunguza maumivu ya bei za mbolea na kwa sasa ni vitendo na baadhi ya mikoa zoezi limeshaanza kufanyika na watu wamejitokeza kwa wingi ili kusajiliwa.

Alibainisha kipindi cha nyuma kilio kikubwa kwenye sekta ya kilimo ni ufinyu wa bajeti ya kilimo sekta ambayo imeajiri asilimia 70 ya Watanzania ikilinganishwa na mzigo mkubwa wa kuzalisha chakula pamoja na malighafi za viwandani.

"Kutokana na jitihada za mheshimiwa Rais kupitia Wizara ya Kilimo bajeti ya kilimo mwaka huu wa fedha Sh. bilioni 751 imetengwa ambapo Sh. bilioni 631 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo ni ongezeko la asilimia 300, ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/21 ilikuwa Sh. bilioni 229 huku miradi ya maendeleo ikiwa Sh. bilioni 150 tu," alisema.

Alisema uhai wa kilimo endelevu ni utafiti wa kina ambapo bajeti yake imepanda kutoka Sh. bilioni 7.3 (2020/21) hadi Sh. bilioni 40.7 kwa mwaka huu wa fedha (2022/23).

Alisema kwenye bajeti ya uzalishaji mbegu imepanda kutoka Sh. bilioni 5.42(2020/21) hadi Sh. bilioni 43.03 (2022/23).

"Tumeshuhudia ugawaji mzuri wa ruzuku za mbegu za alizeti kwa wakulima ambapo gharama zake zimekuwa Sh. 3,500 tu kwa kilo tofauti na bei ambayo haina ruzuku ni Sh. 7,000 hadi 8,000 kwa kilo, kwa hiyo hii imewawezesha wananchi wengi kulima zao hilo kwa wingi ambayo imeongeza uzalishaji wa mafuta ya kula," alisema.

Alimwomba Rais Samia kukutana na wakulima wa sekta hiyo ili kupata mawazo na maoni yao huku akiahidi kuwa wapo pamoja naye na wanaamini kupitia uongozi wake kilimo kitapaa kwa vitendo.





# Watoto 1,700 waripotiwa kupoteza maisha miaka 3

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

ZAIDI ya watoto 1,700 wamefariki dunia mkoani Songwe katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo mama zao kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua huku kukiwa na upungufu mkubwa wa damu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Akitoa takwimu za vifo vya mama na mtoto juzi, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Sogwe, Dk. Boniface Kasululu, alisema watoto waliopoteza maisha ni wale wenye umri wa kati ya siku 0 hadi saba.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa wajawazito 91 nao walipoteza maisha wakati wa kujifungua katika kipindi hicho kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo upungufu wa damu wakati wa kujifungua.

"Mwaka 2019 wajawazito waliofariki dunia walikuwa 31, mwaka 2020 walikuwa 23 na mwaka 2021 walikuwa 28 na kuanzia mwezi Aprili hadi Juni 2022, vifo vilikuwa tisa, hali hii siyo nzuri hata kidogo, jitihada za makusudi zinahitajika.

"Watoto 1,736 wamefariki dunia wenye umri wa kuanzia siku 0 hadi saba ambapo mwaka 2019 watoto 549 walifariki dunia, mwaka 2020 watoto 515, mwaka 2021 watoto 468 na mwaka 2022 kuanzia Januari hadi Juni watoto 204," alibainisha.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Kasululu alisema Mkoa wa Songwe umejipanga kuzuia vifo vya mama na mtoto vinavyotokana na upungufu wa damu pindi wanapofanyiwa upasuaji kwa kuhakikisha damu salama inapatikana saa 24.

Alisema kikao cha wadau wa afya kimefanya tathmini ili kubaini upungufu katika utekelezaji wa vifo vya mama na mtoto vinavyosababishwa na uhaba wa damu kwenye benki ya damu sambamba na kukosekana kwa huduma hiyo ndani ya saa 24.

Alisema vifo hivyo vinaonyesha wajawazito wengi walipoteza damu nyingi wakati wa kujifungua na kwamba tatizo hilo linachangiwa na vituo vya kutolea huduma kutokuwa na damu ya kutosha.

Alisema ni muhimu wataalamu wa afya kwenye maeneo yao kutoa taarifa za ukosefu wa damu salama kwenye benki ya damu ili kuokoa maisha ya wajawazito wanaojifungua ambao wanabainika kuwa na uhitaji wa damu.

Pia aliwaagiza waganga wakuu wa halmashauri kukusanya damu mara kwa mara kwa watu ambao wako tayari ili kuwa na akiba ya kutosha ya damu kwa ajili ya huduma za dharura kwa mjamzito.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, Happiness Seneda, alisema serikali imejitahidi kuboresha mazingira ya kutolea huduma za matibabu na inasikitisha kuona kuna idadi kubwa ya vifo vya mama na mtoto.

Alimtaka Mganga Mkuu kuhakikisha kila kituo kinachotoa huduma ya dharura ambacho kinafanya upasuaji, kinakuwa na wataalamu wote wanaotakiwa kama vile mtaalamu wa kutoa dawa ya usingizi, madaktari wa kutosha na vifaa vya kutosha kutoa huduma za matibabu.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu maandalizi ya sensa ya watu na makazi iliyoanza leo nchini kote. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wenye ulemavu wapewa ajira sensa watu, makazi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imeajiri maofisa wanne wenye ulemavu watakaoshiriki kwenye sensa ya watu na makazi inayofanyika leo nchini.

Maofisa hao wameajiriwa kwa ajili ya kurahisisha kuwahesabu watu wa kundi hilo pamoja na kuhakikisha wanashirikishwa kwenye shughuli za maendeleo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alibainisha hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya sensa, akisisitiza wameshirikisha makundi yote tangu hatua za awali.

Alisema makarani wawili ambao ni wakalimani watashiriki sensa ya watu na makazi kwa kuhakikisha wanakusanya taarifa zote za watu wenye matatizo ya kusikia na kuongea.

Alisema halmashauri hiyo pia imeajiri mtaalamu wa TEHAMA mwenye ualbino pamoja na mlemavu wa viungo ambaye pia yuko kwenye kundi la makarani wa sensa.

"Maandalizi ya sensa yamefikia hatua nzuri, makarani wamejiandaa kikamilifu kuwahudumia wakazi wote wa Wilaya ya Mbeya, muhimu ni wananchi katika maeneo yao kutoa ushirikiano ili tukamilishe kazi hii kwa maendeleo ya taifa letu," alisema Dk. Chuachua.

Alisema wilaya hiyo ina makarani 3,306 ambapo kati ya hao, wakusanya taarifa na wataalamu wa TEHAMA 66 na kwamba kata 64, vijiji 140 na mitaa 181 itahesabiwa.

Aliongeza kuwa tayari wakusanya taarifa wameshafanya ukaguzi wa mipaka ya kazi na kukagua dodoso la sensa kwa ajili ya kuanza kuhesabu watu na makazi.

Mratibu wa Sensa ya Watu na Makazi Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Cosmas Kyovecho, alisema zaidi ya nyumba 300 za kulala ambazo zimesajiliwa zitashiriki kazi hiyo.

Kiongozi wa timu ya sensa ya watu na makazi kutoka Kituo cha ADEM, Dk. Erick Ngwega, alisema kwa kuzingatia mafunzo waliyoyapata, watafanikisha kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa.

# Wazindua programu ya kuboresha malezi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umezindua Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) inayolenga kuboresha malezi ya msingi ya watoto kupitia vipengele vya afya bora na lishe kamili.

Programu hiyo pia inalenga kuimarisha ulinzi na usalama, malezi yenye mwitikio, kujifunza na uchangamshaji wa awali wa watoto katika umri wa chini ya miaka mitano.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alizindua programu hiyo mwishoni mwa wiki, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera.

Madito aliihimiza jamii kuwekeza zaidi kwenye malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto ili kujenga msingi imara wa ukuaji timilifu wa watoto watakapofikia umri wa utu uzima.

Madito aliyataka makundi yote ndani ya jamii mkoani hapa kuhakikisha yanashiriki kwenye utekelezaji wa programu hiyo kwa maelezo kuwa huo ndiyo mwanzo wa taifa lolote kuwa na jamii iliyo kamilifu.

Aliyataja baadhi ya matatizo yanayotokana na jamii kutowekeza kwenye umri mdogo wa watoto ni pamoja na kuwapo kwa watumiaji wa dawa za kulevya na jamii inayojihusisha na biashara ya ngono.

"Hii ni programu jumuishi, hivyo hatutarajii kundi lolote kwenye jamii liachwe nyuma, ndiyo maana mliopo humu kila mmoja ana taaluma tofauti, kila aliyepo hapa, hajaalikwa kwa bahati mbaya, amealikwa kwa makusudi," alisisitiza Madito.

Alisema utaandaliwa utaratibu wa kupima utekelezaji wa mpango huo kila baada ya muda fulani ili kuona ufanisi wake na kupima utekelezaji wa majukumu ya kila mdau.

Ofisa Miradi wa Shirika lisilo la kiserikali la CRS, Neema Haule, aliipongeza serikali kwa kuzindua programu hiyo huku akiwataka wadau wote kushirikiana kwenye utekelezaji wake.

Awali akitoa maelezo ya programu hiyo, Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Salome Francis, aliutaja Mkoa wa Mbeya kuwa wa saba kuzindua programu hiyo tangu ilipozinduliwa kitaifa Desemba mwaka jana.

Salome alihimiza mikoa iliyosalia kuhakikisha inashirikisha wadau muhimu wote kwenye uzinduzi wa programu hiyo ili kuwezesha kuwapo kwa uelewa wa pamoja kwenye utekelezaji wake na kuwezesha matokeo chanya yanayotarajiwa.

"Huu mpango ni muhimu sana kwa taifa letu, tunaendelea kuuzindua kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu ili kuhakikisha tunatengeneza kizazi bora kwa ajili ya maendeleo ya taifa," alisema Salome.

Mmoja wa waandishi wa habari vinara wa habari za makuzi na malezi ya watoto kupitia Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari (UTPC), Joachim Nyambo, aliwahimiza waandishi wa habari wenzake kushiriki kuhamasisha kutoa elimu kwa jamii.

Nyambo alisema kundi la watoto limesahaulika kwenye kazi za uandishi wa habari na hivyo kulifanya kuwa nyonge na lisilo na utetezi wa uhakika ndani ya jamii na kuendelea kukabiliwa na vikwazo vingi.

Alisema ni kupitia kalamu za waandishi wa habari, watoto nchini watakuwa na maisha yanayostahiki kwa jamii kutambua haki zao za msingi ikiwamo usimamizi ili kupata afya bora, ulinzi na usalama wao.



# Taasisi yahimiza ulinzi kwa watoto

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Taasisi ya Nuru Zanzibar, Zainab Kombo Shaib, amesema ulinzi kwa watoto dhidi ya vitendo vya udhalilishaji ni wajibu wa kila mtu ili kuwekeza katika ustawi bora wa jamii.

Zainab ambaye ni Mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alibainisha hayo jana kwa nyakati tofauti katika ziara yake ndani ya Wilaya ya Mkoani alipokuwa anahitimisha ziara yake kisiwani Pemba, akiwasalimia, kuwafariji na kuwapa misaada wananchi, wakiwamo watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu.

Alisema wimbi la vitendo vya ukatilli nchini ni adui wa moja kwa moja wa maisha ya watoto na ustawi wa jamii na linadhoofisha kwa kiasi kikubwa maendeleo katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Aliwashauri watoto kutokuwa wasiri wanapokabiliwa na tishio lolote, bali wawafichue wale wote wanaowafanyia vitendo vibaya.

"Sambamba na haya, tutambue kwamba ni wajibu wetu sote wazazi kuacha muhali wa kuwaficha wahalifu wa vitendo hivyo vya ukatili kwa kuhofia lawama za kifamilia au jamii," alisema.

Pia aliwataka wazazi kutowatumia au kuwaruhusu watoto kujihusisha na ajira za utotoni.

"Kipindi hiki cha uchumaji wa karafuu, baadhi ya watoto wanaonekana katika kazi hizi kwa lengo la kujipatia fedha, ila msimu ukiisha wataanza kujikita katika vitendo vya uhalifu ili tu waendelee kupata fedha, hili ni kosa la wazazi na wanaowaajiri na inabidi likemewe," aliagiza.

Akizungumzia suala la usajili wa watoto yatima unaoendelea katika taasisi yake, mwenyekiti huyo alisema jambo hilo ni muhimu na litasaidia kuwapatia huduma kwa ufanisi zaidi pamoja na kuwahamasisha wafadhili.

"Wanaojitolea kuwafadhili watoto yatima wanakuwa na dhamira njema, hivyo kunahitajika utaratibu wa wazi ili kuwajengea imani zaidi ya kuwasaidia walengwa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mkoani, Khatib Juma Mjaja, alisema jamii yake ni miongoni mwa maeneo yenye idadi kubwa ya watoto yatima na wenye mahitaji maalum, hivyo ujio wa Nuru Foundation chini ya mwenyekiti wake huyo ni faraja na msaada mkubwa kwao.

Mjaja aliwataka viongozi kuwa karibu na jamii ya wenye uhitaji, hususan watoto yatima, ili kuwajengea imani na furaha na kuwaepusha kujiingiza katika makundi ya kihalifu.

# Makamu wa Rais ataka ushirikiano vyombo ulinzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amemtaka Brigedia Jenerali wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) Kanda ya Zanzibar, Said Khamis Said, kuimarisha ushirikiano na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

Hemed aliagiza hayo jana ofisini kwake Vuga, Zanzibar alipokutana na kufanya mazungumzo na kiongozi huyo alipofika kujitambulisha.

Alisema wananchi wa Zanzibar wana imani kubwa na JWTZ kwa utendaji wake unasababisha wananchi kuishi bila hofu kwa sababu wanajua kuwa nchi ipo katika mikono salama.

Alimtaka Brigedia Jenerali Said kusimamia na kuongeza ushirikiano baina ya JWTZ na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha Tanzania inabaki salama.

Alisema jeshi hilo ni nguzo tegemezi, hivyo lazima kulinda miundombinu iliyopo nchini kwa maslahi ya Watanzania.

Brigedia Jenerali Said alisema ataendeleza mazuri yote yaliyoachwa na watangulizi wake kwa lengo la kuhakikisha Tanzania na mipaka yake yote inabaki salama muda wote.

Alisema jeshi hilo litaendelea kulinda miundombinu iliyoko kwa ushirikiano na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ili nchi ibaki salama.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Nuru Zanzibar na Mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Zainab Kombo Shaib, akisalimiana na Mzee Yusuf Othman wa Kijiji cha Mwambe, Mkoa wa Kusini Pemba, wakati wa ziara yake juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waomba kukosolewa waimarishe utendaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Shabaan Ali Othman, amesema uongozi wa wizara yake uko tayari kukosolewa na kupokea maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa huduma zinazotolewa na wizara hiyo.

Kiongozi huyo alitoa kauli hiyo jana wakati wa kikao cha majumuisho kilichofanyika ukumbi wa wizara hiyo baada ya kamati hiyo kufanya ziara sehemu mbalimbali ya utekelezaji wa miradi inayotekezwa na wizara hiyo kupitia idara na taasisi zake.

Shabani alisema wizara yake iko tayari kukosolewa kwa iliyokosea katika utendaji pamoja na kupokea maelekezo ili kuleta ufanisi katika kuwatumikia wananchi.

"Kwanza, ninawapongeza watendaji wote, hasa ninampongeza Katibu Mkuu wangu Kilangi, kama wizara tumepokea maelekezo ya kamati, tutayatekeleza kama tulivyotumwa. Ninaomba kamati isisite kutukosoa zaidi, ninaona kamati imetoa ushauri mzuri katika kutekeleza majukumu yetu, tumeyapokea," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema wizara yake itaongeza kasi katika kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maji na nishati pamoja na kuangalia upya mikataba ya makandarasi kwa lengo la kumaliza miradi hiyo kwa wakati ili kuwaondolea usumbufu wananchi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Abdallah Rashid Aballah, aliutaka uongozi wa wizara hiyo kukamilisha miradi kwa wakati ili kutimiza ahadi ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, aliyowaahidi wananchi katika huduma ya maji na nishati kwa kuwa miaka mitano siyo mingi, hivyo lazima ahadi zake zitekelezwe.

Alisema katika shida walizoziona kupitia utekelezaji wa miradi ya maji, wameshatoa maelekezo ikiwamo kushirikiana na wakazi wa eneo husika wakati wa kufanya utafiti ili kuepusha migogoro isiyo na ulazima.

Alisema kamati yake imeipongeza wizara hiyo ambapo imejionea wenyewe vifaa vya miradi ya umeme ambavyo vimeanunuliwa na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) pamoja kuona maendeleo ya miradi ya maji ikiwamo uchimbaji wa visima, ujenzi wa matangi na utandazaji wa mabomba ya maji kwa Unguja na Pemba.

Katibu Mkuu wizarani huko, Joseph Kilangi, aliwasilisha ripoti ya utekezaji wa wizara ya kwa kipindi cha Februari hadi Juni 2022 ikiwa na mafanikio na vikwazo vilivyowakabili katika utekelezaji wa miradi ya maji na umeme, vikijumuisha vifaa kutofika kwa wakati hali ambayo ilisababisha baadhi ya miradi kuchelewa.

Alisema hivi sasa vifaa ikiwamo mita, mabomba ya maji, vimeshafika na kazi inaendelea vizuri na watendaji wa wizara yake wanafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu ili ufanisi upatikane katika kutekeleza miraji ya mendeleo.

Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Salha Mohammed Kassim, alisema watendaji wake wanafanya kazi kwa usimamizi mkubwa japo kuna ukosefu wa wataalamu katika baadhi ya maeneo, hivyo anahitaji wahandisi na mafundi ili kuongeza kasi ya utendaji katika huduma ya maji.

"Ninaomba serikali kuwekeza elimu kwa vijana katika fani ya uhandisi, wakati mwingine nalazimika kuazima wataalamu kutoka Tanzania Bara kwa sababu nimetafuta hapa nimekosa," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**UPENDO DUNFORD KACHENGA** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **S0243-0035** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **ST.LUISE MBINGA GIRLS SECONDARY** mwaka **2012**,na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1187-0699** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **ST.MARY GORETI SECONDARY** mwaka **2015.**
Taarifa ya polisi **IRI/IRI/RB/331110/2022.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**UPENDO DUNFORD KACHENGA** anatangaza kupotelewa na vyeti,cheti cha chuo cha **SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE** chenye namba **FCS/D/2015/0010** kilichotolewa mwaka **2018** na **TRANSCRIPT** ya chuo cha **SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE** yenye namba **FCS/D/2015/0010** iliyotolewa mwaka **2018**,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi tarifa **IRI/IRI/RB/331110/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**BEN SWILLAH** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma; cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 5873-0076** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SONGWE SECONDARY SCHOOL mwaka 2009** na cheti cha chuo cha **ORDINARY DIPLOMA IN GEOMATIICS** chenye usajili namba **ARI/MG/NTA4/1026** kilichotolewa na **ARDHI INSTITUTE MOROGORO** mwaka **2016.** Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: GE/TR/RB/2596/2022**

## CHANGE OF NAMES



**BY THIS DEED,** I undersigned **UFOOLWANDE AIKAELI KIMARO** of P. O. Box 772 Arusha Tanzania, formerly known as **UFOOLWANDE ONESMO ULOTU** as it appears in my national identity card **No.19620927731060000215** and my many other documents, **NOW THEREFORE, I DO HEREBY DENOUNCE** and **ABANDON** the use of my former names of **UFOOLWANDE ONESMO ULOTU** and in **LIEU** thereof I do assume from the date thereof the names of **UFOOLWANDE AIKAELI KIMARO**
**AND I HEREBY DECLARE** that I shall in future in all records, deeds and instruments in writing and in all actions and proceedings in writing and transaction upon all occasions whatsover,use and sign the assumed names
**AND I HEREBY** authorized and request all persons to address me by such assumed names of **UFOOLWANDE AIKAELI KIMARO** instead of the names denounced
I, the said **UFOOLWANDE AIKAELI KIMARO** make this declaration conscientiously, believing the same to be true and in accordance with the law of united republic of Tanzania
**IN WITNESS WHEREOF** have executed this deed on the **05th** day of **AUGUST, 2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(MCA/63)**
**Katika mahakama ya MWANZO MULEBA MJINI wilaya ya MULEBA**
**MADAI YA TALAKA**
**JAMHURI kwa AMOSI SILASI WA IRINGA MBUYUNI**

Unaamrishwa na **JAMHURI** uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya **JUMATANO** tarehe **31/08/2022 saa 2:00** asubuhi kuwa na mdaiwa katika shauri lililoko mbele ya mahakama hii ukifika usiondoke bila ya ruhusa ya mahakama na unaonywa kwamba usipuuze wito huu.ukipuuzia wito huu bila udhuru wa maana hati itatolewa kukulazimisha kuhudhuria.
Hati hii inatolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe **5/08/2022**
Kuitwa shaurini hii kwa maombi ya **ANNA MUSSA.**

## TANGAZO LA NOTISI MDAIWA SUGU

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi ya siku Sitini (60) kwa ndugu Maya Juma Selemani kulipa deni la mkopo unalodaiwa kwa kumdhamini Hamisa Ally Haji ambaye ameshindwa kulipa deni la mkopo kulingana na makubaliano ya mkataba.

Notisi hii itatumika kuanzia tarehe ya Tangazo hili gazetini.

Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa dhidi yako endapo utashindwa kulipa deni hili ndani ya muda ulioainishwa( siku sitini).

Ikiwa ni pamoja na kuruhusu dalali kuuza mali zako ambazo zimetumika kama dhamana ya mkopo huu.

**Kwa Mawasiliano piga:**
**+255 222774742-3/0718068335**
**Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SALLAH AHMED HUWEL**
Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **FUSO MITSUBISHI** yenye namba za usajili **T546ANK CHASSIS NAMBA FK618K513001**
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**POLISI TAARIFA:**
**IRI/IRI /RB332497/2022**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 86 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late: DEOGRATIUS CHARLES KWIYUKWA BY 1. DORICE LEONIDAS RUGAKIRA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 30 day of AUGUST.........2022
Dated at MOROGO this 16 day of AUGUST.........2022

**RESIDENT MAGISTRATE**

**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL**
**FOR MARA, AT MUSOMA**

**APPLICATION NO.178 OF 2020**

**PETER PAUL MAGANGA....................................APPLICANT**

**VERSUS**

**THE REGISTERED TRUSTEES**
**OF AGAPE SANCTUARY ......................... RESPONDENT**
**CHURCH INTERNATIONAL**

**SUMMONS/ NOTICE**

**TO,**
**THE REGISTERED TRUSTEES**
**OF AGAPE SANCTUARY**
**CHURCH INTERNATIONAL**

The above mentioned applicant has instituted a suit in his Tribunal, against you, particulars of which are mentioned in a copy of the application which is obtainable from the registry of this Tribunal. **YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS TRIBUNAL** in person (s) or by recognized agent(s) for judgment on 26th August, 2022 at 08:00am in the forenoon.
**TAKE NOTICE THAT;**
In default of your appearance on the said day, the above mentioned suit shall be mentioned and determined in your absence.
Given under my hand and seal of this Tribunal this............, day of.....................2022.

Elias Kitungulu
Chairman
The District Land and Housing Tribunal – Mara

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATHIAS STEPHEN CHARLES**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T385 BJV (Toyota corolla spacio), ENGINE NO. 1ZZ2202322,CHASSIS NO. ZZE1223107849,** yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0716730756**
**MOR/MOR/RB/332988/2022.**

## NGOMENI ENTERPRISES

**NOTISI YA SIKU NA NNE (14) YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.**

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na crdb bank makao makuu Dar es salaam tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) tu ili uweze kulipa deni lako lote unalodaiwa. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA / MAHALI | TAREHE/ MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | ARNOLD DOMINIC NYANGE / FORTUNATA ALPHAXAD MAGOMA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO GOBA MTAMBANI YENYE HATI NO. 144568 NA 145667 KITALU M | 19.9.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2. | LIGHTNESS KITENGE | NYUMBA YA MAKAZI - KITUNDA | 6.9.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3. | GODFREY ELIA MATAJI | NYUMBA YA MAKAZI – CHANIKA KWA ZOO | 9.9.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA. |

**MASHARTI YAMNADA.**
1. Dhamana itauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya asilimia 25 ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na asilimia 75 atalipa ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la asilimia 75 katika muda uliopangwa hapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyuma na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**MAWASILIANO:**
**CRDB BANK PLC, HEAD QUARTER. NGOMENI ENTERPRISES, DSM.**
**SIMU: 0719974916/ 0784252048**

**FAGIO BROKERS & AUCTIONEER CO. LTD**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**KWA AMRI YA MAHAKAMA KUU KANDA YA MBEYA , TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA SHULE (MLIMA MBEYA SECONDARY SCHOOL) ILIYOPO PLOT NA.1350 BLOCK 'M' FOREST. MNADA UTAFANYIKA SIKU YA JUMATANO TAREHE 24/8/2022 KUANZIA SAA 5:00 KAMILI ASUBUHI.**

**MASHARTI YA MNADA.**
1. Mshindi atalipa 25% ya bei na baki ilipwe ndani ya siku 14 tangu tarehe ya mnada. Kushindwa kulipa baki hiyo, fedha hazitarudishwa na mnada utarudiwa.
2. Mnunuzi atapewa cheti cha manunuzi (certificate of sale) na mahakama kama mmiliki halali wa mali aliyonunua.
3. Gharama za kubadili umiliki (Transafer of ownership) na gharama nyingine zinazohusiana na umiliki ni za mnunuzi mwenyewe.

**MAWASILIANO**
**0786606041/0757727741**

**Kwa Habari Motomoto Usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Waziri wa zamani afariki gerezani Guinea

**CONAKRY,** GUINEA

WAZIRI wa zamani wa nchini Guinea, Lounceny Camara, aliyefungwa jela na utawala wa kijeshi wa nchi hiyo amefariki gerezani baada ya afya yake kutetereka kwa muda.

Lounceny Camara (62), ni miongoni mwa mawaziri wa zamani na maofisa waandamamizi walioshtumiwa ubadhirifu wa pesa za umma na kufungwa jela baada ya jeshi kumwondoa madarakani Rais wa zamani Alpha Conde mwaka uliopita.

Hayo yalibainishwa jana na kaka wa marehemu na kubainisha kuwa Camara alipatwa na kiharusi Ijumaa ya wiki iliyopita na alifariki hospitalini jioni iliyofuata.

Alisema ilipobainika kuwa Camara anatatizo la kiafya familia yake ilikata rufani mahakamani ili aruhusiwe kusafiri nje ya nchi kupata matibabu, lakini rufani hiyo haikufanikiwa.

"Camara alikuwa tayari amelazwa hospitali mara moja kabla ya kufungwa kwake, mapema mwezi Mei baada ya kufungwa jela," alisema.

Waziri wa Sheria, Charles Alphonse Wright alisema katika taarifa iliyosomwa na vyombo vya habari vya nchini humo kwamba Camara alipata matibabu aliyohitaji katika hospitali ya Chuo Kikuu cha Conakry.

Shirika linalotetea haki za binadamu 'Amnesty International' ambalo limekuwa likikosoa vikali hali ya haki za binadamu nchini Guinea, lilisema mwezi Februari mwaka 2021 kwamba magereza nchini humo yanajulikana kwa kudhulumu haki za wafungwa.

Camara alikuwa amefunguliwa mashtaka ya ubadhirifu wa pesa za umma na mashtaka mengine yanayohusiana na ufisadi, alikuwa mwanachama mkuu wa Chama cha Alpha Conde.

**VOA**

# Odinga atinga mahakamani kupinga matokeo ya uchaguzi

**NAIROBI,** KENYA

MGOMBEA wa urais wa Chama cha Muungano wa Azimio, Raila Odinga, amewasilisha rasmi ombi la kupinga uchaguzi wa William Ruto kuwa rais mteule.

Kwa mujibu wa BBC, kesi hiyo iliwasilishwa jana na mawakili wa Raila walioongozwa na wakili James Orengo katika mahakama ya upeo ya Milimani.

Wakili wa Muungano wa Azimio, Daniel Maanzo, alisema kikosi cha mawakili wa Muungano wa Azimio tayari kimewasilisha kesi hiyo mtandaoni na kwamba watawasilisha stakabadhi zinazohitajika mahakamani wakati wowote kufikia sasa.

"Tumewasilisha kesi hiyo kupitia mtandao huku tukisubiri kuleta stakhabadhi ili mahakama hiyo iweze kuthibitisha ombi hilo, tuna hadi saa nane lakini naweza kuwahakikishia kwamba kila mtu yuko tayari, kundi la mawakili linaendelea kukusanya nakala za kesi hiyo na zinatarajiwa mahakamani muda wowote kuanzia sasa," alisema Maanzo.

Aliongeza kuwa kufuatia hatua ya kuwasilisha kesi hiyo mahakamani, Muungano wa Azimio una hadi tarehe 23 Agosti (leo), kukikabidhi Chama cha UDA, rais mteule na Tume ya Uchaguzi IEBC malalamiko hayo.

Pia ilielezwa kuwa IEBC itakuwa na siku nne kuwasilisha majibu yao katika mahakama ya upeo, kwamba hiyo itafungua njia ya kusikilizwa kwa ombi hilo na majaji wa mahakama ya upeo siku saba baada ya kuwasilishwa Agosti 29.

Majaji wa mahakama ya upeo wakiongozwa na Rais na Jaji Mkuu Martha Koome watakuwa na muda wa hadi Septemba 4, kutoa uamuzi wao kuhusu ombi hilo.

Kulingana na kifungu cha 140 cha Katiba ya Kenya 2010, mahakama kupitia kura ya majaji wengi inaweza kuunga mkono au kubatilisha uchaguzi wa urais iwapo ushindi wa Ruto utaidhinishwa, ambapo ataapishwa siku saba baada ya uamuzi huo kutolewa, uamuzi unaopingana na kutasababisha kurudiwa kwa uchaguzi.

Matokeo ya uchaguzi yalitangazwa na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi IEBC yalisema kwamba mgombea wa Chama cha UDA ndiye aliyeshinda uchaguzi kwa asilimia 50.49 huku mpinzani wake wa karibu Raila Odinga akipata asilimia 48.85.

Hii ni mara ya tano kwa Raila Odinga kuwania wadhifa huo na mara ya tatu kupinga matokeo ya uchaguzi ya urais kupitia mahakama ya upeo, baada ya kuwasilisha pingamizi katika uchaguzi wa 2 mwaka 2013 na 2017.

Mwaka 2017, mahakama ya upeo iliagiza marudio ya uchaguzi, uchaguzi ambao ulisusiwa na Odinga ambaye alipoteza tena kwa rais aliyepo madarakani Uhuru Kenyatta.

Na hayo yakijiri wafuasi wa Muungano wa Azimio wameandamana nje ya mahakama ya milimani ili kuunga mkono azma ya Muungano kuwasilisha kesi hiyo. **BBC**




Mgombea wa Chama cha Azimio la Umoja-One Kenya, Raila Odinga, akiwa katika Mahakama ya Mlimani na jopo la mawakili wake kupinga ushindi wa Rais mteule William Ruto. **PICHA: MTANDAO**

# Marekani, Korea Kusini waanza mazoezi ya kijeshi

**SEOUL,** KOREA KUSINI

MAREKANI na Korea Kusini wameanza kufanya mazoezi ya pamoja ya kijeshi ambayo yanaelezwa kuwa ni ya kwanza kufanyika katika kipindi cha miaka mitano.

Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa jana na DW, msemaji wa wizara ya ulinzi ya Korea Kusini alithibitisha kuanza kwa mazoezi hayo ya kijeshi kama ilivyopangwa, lakini hakutoa maelezo zaidi juu ya idadi ya wanajeshi watakaohusika na vifaa gani vya kijeshi vitakavyotumika.

Pia ilisema vyombo vingine vya habari vimeripoti kwamba mazoezi hayo yatahusisha vifaru, ndege na meli za kivita na maelfu ya wanajeshi.

Rais wa Korea Kusini, Moon Jae-in, alisema mazoezi hayo yatakuwa mwanzo wa serikali kupanga upya maandalizi yake ya kukabiliana na dharura kwa kuzingatia mabadiliko yaliyoko kwenye mfumo mzima wa vita ulimwenguni.

"Vita katika nyakati hizi ni tofauti kabisa na zile za zamani, maadui watafanya mashambulizi ya mtandaoni, kwenye miundombinu ya kitaifa ya habari na mawasiliano na kushambulia maeneo muhimu ya viwanda kama vile bandari, viwanja vya ndege na vinu vya nishati ya nyuklia," alisema na kuongeza;

"Vingine ni vifaa vya teknolojia ya juu na mifumo ya ugavi wa malighafi ili kupunguza uwezo wetu wa kupigana vita, pia suala hili la mazoezi litakuwa mwanzo kwa serikali kupanga upya maandalizi yake ya dharura kulingana na mabadiliko ya mifumo ya vita," alisema.

Taarifa hiyo ilisema Marekani ina wanajeshi karibu 28,500 waliowekwa kambi Korea Kusini, ikiwa ni sehemu ya kukabiliana na vitisho kutoka kwa Korea Kaskazini, iliyojitangaza kuwa taifa lenye nguvu kinyuklia.

Aidha, luteka hizo zilizopewa jina 'Ulchi Freedom Shield' zinahusisha mafunzo ya kompyuta, mazoezi ya pamoja ya kivita na mazoezi makubwa ya kuwalinda raia.

Ilibainishwa kuwa inatarajiwa kukamilika Septemba Mosi mwaka huu, huku ikijiandaa na ukosoaji mkali kutoka kwa Korea Kaskazini baada ya kiongozi wa taifa hilo mara kwa mara kuituhumu Marekani kwa kuandaa uvamizi kupitia mazoezi hayo ya pamoja ya kijeshi na Korea Kusini.

Ilisema Washington na Seoul walikana shutuma hizo na kusisitiza kwamba mazoezi hayo yana nia ya kuboresha uwezo wa kujilinda.

Vile vile wasiwasi wa kikanda unaelezwa kuwa umezidi kuongezeka mwaka huu baada ya majaribio ya mfululizo ya makombora yaliyofanywa na Korea Kaskazini.

Ilisema mazoezi hayo yalipunguzwa na kufutwa kabisa katika miaka ya karibuni kutokana na sababu za kidiplomasia na janga la UVIKO-19.

**DW**

HABARI MICHEZO

# MANDONGA ASHINDA KWA TKO, SASA AMTAKA DULLAH MBABE

Na Saada Akida



ZIKIWA zimepita takriban wiki tatu tangu achezee kichapo kwa KO kutoka kwa Shabani Kaoneka, Bondia wa Ngumi za Kulipwa nchini mwenye mikwala mingi ya kibabe, Karim Mandonga, amekuja kivingine na kujibu mapigo kwa kumchapa Mussa Omary kwa TKO juzi katika ya raundi ya kwanza ya pambano maalum la kuhamasisha sensa itakayofanyika leo huku akitangaza wazi kuwa yupo tayari kupanda ulingoni na Dullah Mbabe.

Mandonga amejizolea umaarufu mkubwa kutokana na mikwala aliyopiga kueleka katika pambano lake na Magambo Christopher ambalo alipoteza kwa KO raundi ya kwanza kabla ya kupigwa tena na Kaoneka kwa TKO licha ya mikwara mizito aliokuwa ameipiga.

Katika pambano hilo maalum la kuhamasisha sensa ambayo inatarajia kufanyika leo, lilifanyika juzi, Jumapili kwenye viwanja vya Leaders Club na Mandonga kushinda katika raundi ya kwanza.

Baada ya ushindi huo, Mandonga alisema kwa sasa ameamua kutumia mifumo miwili tofauti katika kuhakikisha anashinda mapambano yake na kwamba wa kwanza ni kuongea na vyombo vya habari huku wa pili ukiwa ni kutembeza vipigo vya aina yake.

"Sasa hivi nimekuja na mifumo miwili, mfumo wa kwanza ni kuongea na vyombo vya habari, lakini wa pili ni wa kukaa ulingoni na kuwaonyesha mashabiki wangu kuwa 'Mandonga Mtu Kazi' amekusudia jambo gani akiwa ndani ya ulingo, niliyokuja nayo sasa siyo tena ile mtumbwi wa vibwengo ila ni 'mwanaume halii na bahari haikauki'.

"Pambano linalokuja, naenda Mtwara kisha Kigoma halafu namalizia mkoani Morogoro ila katika ngumi kila mmoja ana njia yake ya kuongea, njia ya kweli ni promota peke yake, huyo Dullah Mbabe nishamweleza, yeye Mzaramo na mimi mtoto wa Morogoro, lakini akae akijua Mandonga sina fagio na mtu akijikanyaga naruka naye," alisema Mandonga.

# Geita roho kwatu sare na Azam

Na Adam Fungamwango

KOCHA Msaidizi wa Geita Gold FC, Fred Felix Minziro, amesema ameridhishwa na sare aliyoipata dhidi ya Azam FC kwa sababu aliwaambia wachezaji wake, kama hawatoshinda na kupata pointi tatu, basi wapate angalau pointi moja kwenye mechi hiyo.

Geita Gold ililazimisha Azam kutoka nayo sare ya bao 1-1 juzi usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi ikiwa ni sare ya kwanza kwa timu hizo zote mbili.

Kwenye mechi za ufunguzi, Geita Gold ilipokea kichapo cha mabao 3-0 dhidi ya Simba, huku Azam ikishinda mabao 2-1 dhidi ya Kagera Sugar.

"Mechi haikuwa rahisi, tulicheza kwa presha kwa sababu tulitoka kupoteza mechi dhidi ya Simba kwa mabao 3-0. Ni mabao mengi sana, kwa hiyo nikawaambia vijana wangu kuwa wajitahidi kwenye mechi hii tupate ushindi, na kama si ushindi basi angalau sare tuvune pointi moja kwa sababu Azam ni timu nzuri na imefanya usajili mkubwa na sisi hatukupata mechi nyingi za kirafiki kwenye maandalizi ya kuanza msimu mpya wa ligi.

"Kwa hiyo baada ya mechi ya Simba tuliangalia makosa yetu, tukajitahidi kuyarekebisha na ndiyo maana unaona leo hatukuwa na makosa mengi kama mechi iliyopita." alisema Minziro.

Alisema timu yake imecheza mechi mbili kubwa dhidi ya Simba na Azam, ikipata pointi, hivyo si mbaya, akiahidi mechi zinazofuata atakuwa nyumbani na anatumaini kufanya vema.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdihamid Moallin, alisema wachezaji wake wengi ni wapya, hivyo wanaendelea kujifunza vitu mbalimbali, lakini anaendelea kuyafanyia kazi mapungufu kuelekea kwenye mechi inayofuata dhidi ya Yanga.

"Kipindi cha kwanza tulicheza kwa nguvu, lakini haikuwa hivyo kipindi cha pili. Tuliruhusu bao la faulo, tunaendelea kujifunza, na tunaendelea kuyafanyia kazi makosa yote kabla ya mechi dhidi ya Yanga," alisema Moallin.

Yalikuwa ni mabao ya Tepsi Evance kwa upande wa Azam na Adeyum Suleiman akiisawazishia Geita Gold.

Azam ipo kwenye nafasi ya tano ya msimamo ikiwa na pointi nne, Geita Gold ikiwa nafasi ya 13 na pointi yake moja.

# Coastal kuanza kuiwinda Polisi kesho

Na Shufaa Lyimo

KATIKA kuhakikisha wanajiweka sawa kabla ya Ligi Kuu kurejea tena, wachezaji wa Coastal Union wamepewa mapumziko ya siku tatu kwenda kusalimia familia zao na baada ya hapo watarejea kambini kuendelea kujiwinda na ligi hiyo iliyosimama kupisha Kalenda ya Fifa.

Katika kipindi hiki cha wiki mbili kupisha Kalenda hiyo ya Fifa, Taifa Stars ambayo iliingia kambini juzi, itacheza na Uganda nyumbani na ugenini kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchini Algeria.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka jijini Tanga, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Juma Mgunda, alisema baada ya mchezo wao wa Ligi Kuu Jumamosi dhidi ya Yanga, aliwapa mapumziko mafupi ya siku tatu wachezaji wake.

"Baada ya kumaliza mchezo wetu (katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid) jijini Arusha dhidi ya Yanga, niliwapa mapumziko wachezaji wangu mpaka sensa (ambayo inafanyika leo) litakapomalizika warudi kambini," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema alibaini makosa katika mchezo uliopita jambo ambalo ameahidi kulifanyia kazi katika kipindi hiki cha mapumziko.

Alisema yote ambayo ameyaona hawezi kuyaweka hadharani isipokuwa ataendelea kukaa na kuzungumza na wachezaji wake ili mchezo ujao watakaocheza Septemba 10, mwaka huu dhidi ya Polisi Tanzania yasijirudie tena.

"Baada ya sensa nitaendelea kuwapa mazoezi wachezaji wangu kwa ajili ya kujiandaa kukutana na timu ya Polisi Tanzania, ni mchezo ambao tunatarajia kuwa mgumu," alisema.

Coastal Union ipo nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi hiyo iliyochezwa raundi mbili hadi sasa msimu huu, ikiwa na pointi tatu baada ya kupoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya Yanga na kushinda mchezo wake wa awali kwa bao 1-0 dhidi KMC FC.

## ZISIKUPITE

### ANTONY ATAKA KUTUA UTD
WINGA wa Ajax Mbrazil Antony, anashinikiza kujiunga na Manchester United kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili msimu huu. ***(Goal)***

### PEPE KUNG'OLEWA ARSENAL
KLABU ya Nice inaendelea na mazungumzo na Arsenal kuhusu mkataba wa mkopo wa winga wa Ivory Coast, Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 27. ***(Fabrizio Romano)***

### DE JONG AKOMALIWA
MANCHESTER United pia wanajiandaa kushinikiza kwa mara ya mwisho mwezi huu kumsajili kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25. ***(Marcel van der Kraan, via Express)***

### TANGANGA NA AC MILAN
KLABU ya AC Milan imetumia mbinu nyingine kumnunua beki wa kati wa Tottenham Hotspur, Japhet Tanganga mwenye umri wa miaka 23. ***(Calciomercato)***

### PEDRO ANUKIA NEWCASTLE
NEWCASTLE United wanatumaini kupata uhamisho wiki hii huku klabu hiyo ikifanyia kazi mikataba miwili na kuamini uhamisho wa mshambuliaji wa Watford raia wa Brazil, Joao Pedro mwenye umri wa miaka 20, utawezekana. ***(iNews)***

### UNITED SASA KWA GAKPO
MANCHESTER United sasa wanamwinda winga wa PSV Eindhoven Mholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23, lakini wana uwezekano wa kusajili mmoja wa washambuliaji kabla ya dirisha la usajili kufungwa. ***(Telegraph)***

### WALSH AWINDWA BARCA
KIUNGO wa kati wa Manchester City na England, Keira Walsh mwenye umri wa miaka 25, bado anawindwa na Barcelona. (Sport)

### CIFUENTES AGOMBEWA
LEEDS United na Newcastle zinamfuatilia kiungo wa kati wa Los Angeles FC kutoka Ecuador, Jose Cifuentes mwenye umri wa miaka 23, ambaye anawindwa na Brighton. ***(Sun)***

### REGUILON ATAKIWA LAZIO
LAZIO wanataka kumnunua beki wa kushoto wa Tottenham Hotspur, Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 25. ***(Calciomercato)***

### AURIER AWANIWA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest ina nia ya kumsajili Serge Aurier mwenye umri wa miaka 29. Beki huyo wa kulia wa Ivory Coast ni mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba na Villarreal. ***(Footmercato, via Express)***

### BEDNAREK ATAKIWA VILLA
KLABU ya Aston Villa imewasilisha ofa ya mkopo kwa beki wa kati wa Poland, Jan Bednarek mwenye umri wa miaka 26, kutoka Southampton. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA ATAJA MUDA HAALAND KUPUMZISHWA

**Nitamchezesha Alvarez au Mahrez tutakapoanza kuwa na mechi kila baada ya siku tatu kila mmoja atacheza...**

**NEWCASTLE, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amefichua kwamba, Erling Haaland atapumzishwa punde tu mahitaji ya mechi yatakapoongezeka ili kumlinda dhidi ya majeraha.

Haaland aliwasili City wakati huu wa majira ya joto kama mmoja wa washambuliaji bora katika soka la dunia.

Raia huyo wa Norway, alifunga takriban bao moja kwa kila mechi msimu uliopita akiwa na Borussia Dortmund, lakini alicheza mechi 30 pekee katika mashindano yote kwa sababu ya majeraha.

Kufikia sasa msimu huu, Haaland tayari ameanza michezo yote mitatu ya Ligi Kuu ya England na City, pamoja na Ngao ya Jamii. Lakini City wamekuwa wakicheza mara moja tu kwa wiki.

Baada ya mabadiliko ya mwanzo wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na ushiriki wa City katika Kombe la Carabao kutoka hatua ya raundi ya tatu - Guardiola ana mpango wa kutomtumia vibaya nyota wake namba tisa, ambaye alimaliza dakika 90 dhidi ya Newcastle kwa mara ya kwanza kwenye mchezo wa Ligi Kuu, Jumapili.

"Chakula kizuri, pumziko zuri. Watu wanasema nyumba mpya aliyonunua ina kitanda kizuri. Hakuna cha ziada. Kitu cha muhimu ni kutokuwa na matatizo. Madaktari wamefanya kazi ya ziada tangu alipowasili hapa ili kuepuka majeraha," alisema Guardiola baada ya Man City kutoka nyuma na kupata sare ya mabao 3-3 dhidi ya Newcastle kwenye dimba la St James' Park.

"Kwa sasa ana mchezo mmoja kwa wiki. Nawaambia nyinyi kama tutakuwa na mechi kila baada ya siku tatu ni kwamba, Erling hatacheza.

"Nitamchezesha Julian (Alvarez). Mmoja wa wachezaji wenye upatina mzuri na Bernardo (Silva) na hajacheza hadi leo hii (juzi).

"Riyad (Mahrez) ni mmoja wa wachezaji wengine na hasa kwenye hatua kubwa na leo (juzi) hakucheza. Tutakapoanza kuwa na mechi kila baada ya siku tatu kila mmoja atacheza."

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,025,1

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 23, 24 NA 25 AGOSTI 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/08/22 | 21:45 | Barrow vs Lincoln | 2.76 | 3.32 | 2.43 |
| 02. 23/08/22 | 21:45 | Newport vs Portsmouth | 2.87 | 3.32 | 2.35 |
| 03. 23/08/22 | 21:45 | Stevenage vs Peterborough | 2.96 | 3.31 | 2.30 |
| 04. 23/08/22 | 21:45 | Gillingham vs Exeter | 3.10 | 3.30 | 2.22 |
| 05. 23/08/22 | 21:45 | Norwich City vs Bournemouth | 2.66 | 3.36 | 2.49 |
| 06. 23/08/22 | 21:45 | Forfar Athletic vs Kelty Hearts FC | 2.65 | 3.43 | 2.32 |
| 07. 23/08/22 | 21:45 | Elgin City vs Stenhousemuir | 2.43 | 3.63 | 2.43 |
| 08. 24/08/22 | 03:05 | Guadalajara Chivas vs CF Monterrey | 2.72 | 3.02 | 2.67 |
| 09. 25/08/22 | 20:00 | Sivasspor vs Malmo | 2.72 | 3.33 | 2.48 |
| 10. 25/08/22 | 20:00 | Viking vs Steaua Bucuresti | 2.39 | 3.29 | 2.88 |
| 11. 25/08/22 | 20:00 | Twente vs Fiorentina | 2.77 | 3.28 | 2.47 |
| 12. 25/08/22 | 21:45 | Linfield Belfast vs Rigas Futbola Skola | 2.91 | 3.17 | 2.43 |
| 13. 25/08/22 | 22:00 | Hearts vs FC Zurich | 2.37 | 3.33 | 2.88 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa · vodacom m-pesa · BREAKING · airtel money · ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LEWANDOWSKI AANZA KUKIWASHA LALIGA



**BARCELONA, Hispania**

ROBERT Lewandowski alifunga mabao yake ya kwanza ya ushindani akiwa na Barcelona katika siku yake ya kuzaliwa ya kutimiza umri wa miaka 34, huku klabu hiyo ya Katalunya ikishinda 4-1 dhidi ya Real Sociedad kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumapili.

Mshambulizi huyo wa zamani wa Bayern Munich alifunga bao lake la kwanza baada ya sekunde 47 pekee akiunganisha krosi ya Alejandro Balde.

Ousmane Dembele akafunga bao la pili, kabla ya Lewandowski kufunga la tatu na Ansu Fati akafunga la nne.

Ushindi huo mzuri ulikaribishwa baada ya Barca kuanza Ligi kwa sare ya bila kufungana nyumbani dhidi ya Rayo Vallecano.

Lewandowski alijiunga na Barca msimu wa majira ya joto kwa ada ya pauni milioni 42 akitokea Bayern, ambapo alikuwa amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake, huku mchezaji mwingine mpya aliyesajiliwa, mshambuliaji wa zamani wa Leeds United na Brazil, Raphinha, akitokea benchi kipindi cha pili.

Hata hivyo, Barcelona hawakuweza kumchezesha beki wa kati wa Ufaransa, Jules Kounde kwa kuwa bado hajasajiliwa kwa sababu za kifedha baada ya uhamisho wake kutoka Sevilla mwishoni mwa Julai.

Barca wako katika nafasi ya tano kwenye LaLiga na watacheza na Manchester City katika mechi ya hisani kesho Jumatano, na mchezo wao ujao wa kimashindano ni dhidi ya Valladolid kwenye Uwanja wa Nou Camp, Jumapili.

# Tuchel: Chelsea haihitaji kiungo au mshambuliaji

**LONDON, England**

THOMAS Tuchel amepuuzilia mbali pendekezo kwamba, Chelsea inahitaji kuongeza mshambuliaji au kiungo kabla ya dirisha la usajili kufungwa.

'The Blues' walipata kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Leeds United kwenye Uwanja wa Elland Road, na kuwaacha vijana wa Tuchel wakiwa mkiani mwa jedwali la Ligi Kuu England baada ya mechi tatu.

Washambuliaji watatu wa Chelsea kwa mara nyingine walishindwa kuzifumania nyavu, Raheem Sterling, Mason Mount na Kai Havertz.

Na Tuchel alipoulizwa ikiwa matokeo yalisisitiza hitaji la kuimarisha katika maeneo ya mbele, alijibu: "Hapana, hapana."



Conor Gallagher pia alianza kwa mara ya kwanza akiwa na jezi ya Chelsea pamoja na Jorginho kwenye safu ya kiungo, lakini Muingereza huyo alishindwa kutamba.

Alipoulizwa iwapo The Blues watataka kuimarisha safu yao ya kiungo kabla ya mwisho wa dirisha la uhamisho, Tuchel alisema timu yake ina watu wengi.

"Kiungo mwingine? Tuna Jorginho, N'Golo Kante, tuna Ruben Loftus-Cheek, Conor Gallagher, Mateo Kovacic.

"Wao (Kovacic na Kante) ni majeruhi, ndiyo, ni tatizo. Lakini watarejea. Hawajatoweka."

Katika dakika za mwisho, Leeds walikuwa wamekimbia umbali wa kilomita 11 zaidi ya Chelsea, lakini Tuchel alipuuza wazo kwamba The Blues walishindwa kuendana na juhudi za wenyeji wao.

"Tulifungwa bao la kujifunga na tukatoa sehemu ya urahisi na tukafungwa kirahisi," aliongeza kocha huyo raia wa Ujerumani.

"Hii haina uhusiano wowote na kukimbia kilomita chache, hakuna uhusiano wowote na mtindo wa Leeds. Hatupaswi kuchanganya mambo haya. Tuliweza kumudu staili hiyo."

118,259/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/08/22 | 17:00 | Blackpool vs Bristol City | 2.28 | 3.19 | 3.19 |
| 02. 27/08/22 | 17:00 | Cardiff vs Preston | 2.54 | 3.08 | 2.89 |
| 03. 27/08/22 | 17:00 | Hull City vs Coventry | 2.64 | 3.19 | 2.69 |
| 04. 27/08/22 | 17:30 | GO Ahead Eagles vs Sparta Rotterdam | 2.33 | 3.53 | 2.84 |
| 05. 27/08/22 | 19:30 | Juventus vs Roma | 2.31 | 3.19 | 3.14 |
| 06. 27/08/22 | 19:30 | Cremonese vs Torino | 2.99 | 3.34 | 2.32 |
| 07. 27/08/22 | 21:45 | Spezia vs Sassuolo | 2.99 | 3.39 | 2.29 |
| 08. 27/08/22 | 22:00 | Lens vs Rennes | 2.44 | 3.36 | 2.76 |
| 09. 28/08/22 | 01:00 | Fluminense vs Palmeiras | 2.60 | 3.15 | 2.75 |
| 10. 28/08/22 | 14:00 | Nantes vs Toulouse | 2.40 | 3.27 | 2.88 |
| 11. 28/08/22 | 14:30 | KAA Gent vs Royal Antwerp | 2.34 | 3.43 | 2.89 |
| 12. 28/08/22 | 14:30 | Hannover vs Greuther Furth | 2.79 | 3.39 | 2.43 |
| 13. 28/08/22 | 15:15 | FC Lugano vs St. Gallen | 2.45 | 3.49 | 2.69 |
| 14. 28/08/22 | 16:00 | Aston Villa vs West Ham | 2.37 | 3.24 | 2.99 |
| 15. 28/08/22 | 16:00 | Wolverhampton vs Newcastle | 2.64 | 3.19 | 2.69 |
| 16. 28/08/22 | 16:00 | Nice vs Marseille | 2.48 | 3.33 | 2.73 |
| 17. 28/08/22 | 16:00 | Troyes vs Angers | 2.53 | 3.18 | 2.78 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 23 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5938 | Shakhtar Donetsk vs FC Metalist 1925 | 1.33 | 4.70 | 8.60 |
| 14:15 | 1614 | PS Tni vs Bhayangkara Surabaya Utd | 4.62 | 3.39 | 1.70 |
| 14:15 | 2325 | Pusamania Borneo vs Dewa United | 1.56 | 3.72 | 5.29 |
| 15:00 | 2274 | Zorya Lugansk vs Vorskla Poltava | 2.65 | 3.25 | 2.50 |
| 15:00 | 3055 | Chernomorets Odessa vs Veres Rivne | 2.04 | 3.45 | 3.30 |
| 16:00 | 4151 | Persib Bandung vs Bali Utd Pusam | 2.54 | 2.93 | 2.74 |
| 16:00 | 4849 | Persis Solo vs Persepam MU | 3.60 | 3.25 | 2.01 |
| 17:00 | 2992 | Kolos Kovalivka vs FC Kryvbas Kriviy Rih | 2.80 | 3.35 | 2.36 |
| 17:20 | 3181 | Al Rayyan SC vs Al Ahli Doha SC | 1.89 | 3.64 | 3.39 |
| 18:30 | 1018 | Kerho 07 vs Pif Jalkapallo | 1.66 | 3.74 | 4.33 |
| 18:30 | 2265 | Arab Contractors vs Farco FC | 2.05 | 2.71 | 4.61 |
| 18:30 | 5517 | Smouha Club vs El Gouna | 2.03 | 3.31 | 3.56 |
| 18:30 | 5659 | Klubi 04 vs FC Honka/Akatemia | 1.57 | 4.32 | 4.32 |
| 19:00 | 2870 | Apoel Nicosia vs Djurgardens IF | 2.33 | 3.28 | 2.98 |
| 19:00 | 5720 | CSA Steaua Bucuresti vs Miercurea Ciuc | 2.18 | 3.05 | 3.20 |
| 20:00 | 4373 | Orebro SK vs Skovde Aik | 2.08 | 3.47 | 3.42 |
| 20:00 | 4665 | Orgryte IS vs Norrby IF | 2.89 | 3.25 | 2.46 |
| 20:30 | 4574 | Cape Town City vs Kaizer Chiefs | 2.90 | 2.85 | 2.60 |
| 21:00 | 1674 | KV Vesturbaer vs UMF Grindavik | 2.85 | 3.63 | 2.11 |
| 21:00 | 2333 | Zamalek vs El Ittihad Alexandria | 1.43 | 4.32 | 7.03 |
| 21:00 | 2704 | National Bank vs Al Masry Club | 3.63 | 3.02 | 2.14 |
| 21:00 | 3584 | Walsall vs Charlton | 3.02 | 3.32 | 2.26 |
| 21:00 | 4354 | IF Vestri vs Fjolnir | 2.65 | 3.53 | 2.28 |
| 21:30 | 1318 | Sheffield Wed vs Rochdale | 1.46 | 4.44 | 6.05 |
| 21:30 | 5086 | Shrewsbury vs Burnley | 3.33 | 3.38 | 2.09 |
| 21:45 | 1032 | Bolton vs Aston Villa | 6.42 | 4.51 | 1.43 |
| 21:45 | 1128 | Stevenage vs Peterborough | 2.87 | 3.32 | 2.35 |
| 21:45 | 1139 | Crusaders Belfast vs Portadown FC | 1.19 | 5.91 | 10.84 |
| 21:45 | 1147 | Bradford City vs Blackburn | 3.41 | 3.41 | 2.05 |
| 21:45 | 1329 | Watford vs MK Dons | 1.52 | 4.14 | 5.65 |
| 21:45 | 1372 | Fleetwood Town vs Everton | 6.45 | 4.53 | 1.43 |
| 21:45 | 1452 | Newport vs Portsmouth | 2.81 | 3.32 | 2.39 |
| 21:45 | 1529 | Rotherham vs Morecambe | 1.48 | 4.24 | 6.06 |
| 21:45 | 2210 | Stockport vs Leicester | 7.24 | 4.63 | 1.39 |
| 21:45 | 2392 | Carrick Rangers vs Coleraine FC | 3.25 | 3.35 | 2.03 |
| 21:45 | 2489 | Wolverhampton vs Preston | 1.64 | 3.77 | 5.02 |
| 21:45 | 2716 | Norwich City vs Bournemouth | 2.66 | 3.36 | 2.49 |
| 21:45 | 2874 | Kilmarnock FC B vs East Stirling | 1.73 | 3.83 | 3.83 |
| 21:45 | 3250 | Colchester vs Brentford | 10.04 | 5.42 | 1.26 |
| 21:45 | 3375 | Stafford Rangers vs Marine FC | 1.85 | 3.43 | 3.72 |
| 21:45 | 3426 | Crawley Town vs Fulham | 9.67 | 5.64 | 1.26 |
| 21:45 | 3430 | Gillingham vs Exeter | 3.17 | 3.27 | 2.20 |
| 21:45 | 4199 | Derby vs West Bromwich | 3.12 | 3.32 | 2.20 |
| 21:45 | 4899 | Grimsby vs Nottingham | 7.63 | 4.62 | 1.37 |
| 21:45 | 5423 | Oxford Utd vs Crystal Palace | 6.01 | 4.20 | 1.49 |
| 21:45 | 5840 | Cambridge Utd vs Southampton | 7.43 | 4.82 | 1.36 |
| 22:00 | 1973 | Viktoria Plzen vs Karabakh | 2.04 | 3.20 | 3.60 |
| 22:00 | 3544 | Red Star Belgrade vs Maccabi Haifa | 1.76 | 3.71 | 4.11 |
| 22:00 | 4510 | Benfica vs Dynamo Kiev | 1.33 | 4.89 | 8.18 |
| 22:15 | 3761 | HK Kopavogs vs Fylkir | 2.02 | 3.57 | 3.08 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# BABA WA SAMATTA AKUNWA MWANAWE KUREJEA GENK

**Na Hadija Mngwai**



BABA mzazi wa nahodha wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta, mzee Ally Samatta, amesema amefurahishwa na kitendo cha mwanawe huyo kurejea kwa mara nyingine katika klabu yake ya zamani ya KRC Genk, ya Ubelgiji ambapo alijenga ufalme wake kisoka.

Nahodha huyo wa Taifa Stars ambaye alijiunga KRC Genk mwaka 2016 hadi 2020 alipotimkia Aston Villa ya England aliyodumu kwa kipindi cha nusu msimu kabla ya kutolewa kwa mkopo Fenerbahce na baadaye kununuliwa jumla na klabu hiyo ya Uturuki, amerejea kuitumikia timu yake hiyo ya zamani ambayo aliichezea mechi 101 na kuifungia mabao 43.

Kabla ya kutua Genk msimu huu, msimu uliopita aliichezea pia kwa mkopo Royal Antwerp ya Ubelgiji mechi 32 na kufunga mabao matano, akitokea pia Fenerbahce.

Akizungumza na Nipashe jana, Mzee Samatta, alisema kuwa, ni jambo jema kwa mwanawe Samatta kurejea katika klabu hiyo iliyompa umaarufu na kujiwekea historia nzuri kwa kuwa alivyoondoka alivurugwa na kushuka kiwango chake.

"Nimefurahi kuona Samatta amerejea Genk kwa kuwa aliondoka akiwa shujaa kutokana na kuifanyia vizuri klabu yake na hata alivyorejea tuliona jinsi mashabiki walivyomshangilia licha ya kucheza dakika 10 tu.

"Alivyoondoka klabu alizokwenda zilimvuruga sana na kushuka kiwango, hivyo klabu yake hiyo ikaona kwa nini iwe hivyo na kuamua kumrejesha ili waweze kumpika upya na kurejesha historia yake ambayo ilimpeleka Genk, hata mwenyewe amefurahia kurudi hapo na ameahidi kujituma," alisema Mzee Samatta.

# Mbeya City yalia na waamuzi, Singida yajichimbia Arusha

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya juzi kupoteza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Big Stars kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida, Mbeya City imewanyooshea kidole cha shahada waamuzi wa mechi hiyo kwa madai kuwa hawakuwatendea haki.

Kocha msaidizi wa timu hiyo, Antony Mwamlimwa, amesema kulikuwa na matukio mengi kwenye mechi hiyo yalioashiria kuwa waamuzi hawakuwa upande wao, hivyo kipigo cha mabao 2-1 walichokipata siyo kwa sababu timu yao ilizidiwa, bali waamuzi walichangia timu hiyo kupoteza.

"Mpira wa Tanzania ili uendelee unahitaji watu wanaosimamia sheria 17 za mpira uwanjani, unawekeza kwenye timu na unasajili wachezaji wazuri wazoefu ili wakusaidie kupata matokeo mazuri uwanjani, lakini linapokuja tena suala la kusaidiwa na waamuzi au 'figisu' zingine uwanjani haileti picha nzuri, tunawekeza ili kuweza kupata matokeo mazuri na ya baadaye. Tumepoteza, siyo kwa maana tulifanya makosa mengi uwanjani, sisi ndiyo tumeukamata mchezo, lakini tumevunjwa nguvu na wanaosimamisha sheria," alilalama kocha huyo.

Yalikuwa ni mabao ya Wabrazil Dario da Silva kwa penalti na Bruno Gomes, huku Sixtus Sabilo ndiye aliyekuwa wa kwanza kuiandikia Mbeya City bao la kuongoza.

Mbeya City imepoteza mechi hiyo, baada ya kushinda kwenye uwanja huo huo mechi ya kwanza mabao 3-1 dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Kwa upande wa Singida Big Stars, ni ushindi wake wa pili mfululizo baada ya mechi ya kwanza kupata kushinda bao 1-0 kwenye uwanja huo dhidi ya Tanzania Prisons.

Wakati huo, Singida Big Stars inatarajia kuondoka leo Jumanne kwenda Arusha kuweka kambi, baada ya mapumziko kupisha Kalenda ya FIFA, huku wachezaji wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars wakiwa kambini.

Msemaji wa klabu hiyo, Hussein Massanza, amesema kambi hiyo ni maalumu kwa kujipanga zaidi na Ligi Kuu ambayo amesema ni raundi ya pili tu, lakini imechangamka.

Michezo
Jumanne Agosti 23, 2022
Nipashe



## Guardiola ataja muda Haaland kupumzishwa



Mayele Phiri

## Mbio Mayele, Phiri zamwibua Mpole

**Na Adam Fungamwango**

HUKU Reliants Lusajo wa Namungo FC, Moses Phiri (Simba) na Fiston Mayele wa Yanga, wakikimbizana kwenye mbio za ufungaji bora wa Ligi Kuu Bara, mshindi wa Kiatu cha Dhahabu kwenye ligi hiyo msimu uliopita, George Mpole wa Geita Gold, amesema yuko kwenye mkakati wa kubadilisha ubunifu na mbinu za kukabiliana na mabeki wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kutokana na kukamiwa.

Mpole ambaye hajapata bao lolote kwenye mechi mbili za kwanza msimu huu, amesema kwa sasa timu zinajiandaa kisawasawa zinapokwenda kucheza dhidi ya Geita Gold kwa sababu zinajua wanakwenda kucheza mechi ngumu pamoja na kumkaba Mpole.

Hadi sasa Lusajo ndiye yupo kileleni mwa wafungaji bora msimu huu, akiwa amecheka na nyavu mara tatu huku akifukuziwa kwa karibu na Phiri pamoja na Mayele ambao kila mmoja ana mabao mawili.

"Naweza kusema ligi ni ngumu, sisi mechi zote kila timu inajua tunakwenda kucheza na Geita Gold, nakwenda kumkaba Mpole kwa hiyo wanakuwa wako makini sana tofauti na msimu uliopita, pamoja na hayo mimi nitafunga tu, hii inanipa changamoto ya kubadilisha mbinu na ubunifu, tumecheza mechi mbili ugenini baada ya hapa na sisi tunarudi nyumbani, tutafanya vizuri tu," alisema.

Mpole ambaye msimu uliopita alimaliza na mabao 17, amecheza mechi zote mbili za mwanzo msimu huu, timu yake ikichezea kichapo cha mabao 3-0 dhidi ya Simba na ikitoka sare ya 1-1 dhidi ya Azam FC juzi, shukran kwa Adeyum Suleiman aliyeisawazishia kwa mkwaju wa faulo.

# SIMBA KUIVAA ASANTE KOTOKO

## ●●●Ni katika michuano maalum, Yanga yageukia kimataifa...

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Ligi Kuu ikiwa mapumzikoni kupisha Kalenda ya Fifa itakayoisha Septemba 4, mwaka huu, Klabu ya Simba imepokea mwaliko kutoka kwa Klabu ya Al Hilal ya Sudan kushiriki michuano maalum itakayofanyika wiki ijayo.

**Ahmed Ally, Meneja Mawasiliano wa Klabu ya Simba, aliiambia Nipashe jana kuwa wakiwa Sudan, watacheza mechi mbili dhidi ya Asante Kotoko ya Ghana, Agosti 28 na wenyeji Al Hilal Agosti 31 mwaka huu.**

"Mechi hizi za kimataifa tutazitumia kama sehemu ya maandalizi wakati ligi ikiwa imesimama kupisha mechi za kufuzu Fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

"Wachezaji tisa walioitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) inayojiandaa kwa mchezo dhidi ya Uganda, hawatakuwa sehemu ya safari.

"Timu inatarajia kuondoka nchini Alhamisi alfajiri kuelekea Sudan, tayari kuwahi mechi ya kwanza itakayopigwa Agosti 28, dhidi ya Asante Kotoko.

"Baada ya kukamilika kwa mashindano, kikosi kitarejea nchini na Septemba 3 na kitacheza mechi nyingine ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya mabingwa wa Djibouti, AS Arta Solar 7 ambao wako kambini jijini Dar es Salaam wakiwa na nyota kama Alexander Song na Solomon Kalou," alisema.

Ally alisema mwaliko huo ni mwendelezo wa ushirikiano baina yao na Al Hilal ambayo mwaka 2020 waliwaalika katika michuano ya Simba Super Cup.

Wakati hayo yakiendelea Msimbazi, watani wao Yanga wamezungumzia maandalizi ya mechi yao ya awali ya michuano Ligi ya Mabingwa barani Afrika.

Meneja wa Yanga, Walter Harrison, ambaye timu yake itaanzia ugenini dhidi ya Zalan FC ya Sudan Kusini, alisema jana kuwa kufanya kwao vyema kwenye mechi kadhaa kuanzia Ngao ya Jamii hadi sasa, ni hatua za awali za maandalizi hayo, huku matokeo chanya wanayoyapata yakionyesha kuwa wamedhamiria kufanya vizuri mwaka huu.

"Tuna kikosi bora zaidi, kwa mfululizo wa matokeo tunayoyapata kuanzia Ngao ya Jamii hadi michezo miwili ya Ligi Kuu, huku wakati mwingine tukianza kwa kufungwa, lakini tunasawazisha na kufunga bao la ushindi inaonyesha ni jinsi gani wachezaji wako tayari na pia ubora wa kikosi, hivyo inatupa matumaini ya kufanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa.

"Michezo ya ligi ni maandalizi ya awali ya Ligi ya Mabingwa, haya tunayofanya, mechi za ligi tulizocheza na zingine ambazo tutaendelea kucheza ni maandalizi ya mechi ya kimataifa dhidi ya Zalan FC ya Sudan ya Kusini," alisema Harrison.

Yanga imecheza mechi zote mbili za mwanzo za Ligi Kuu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid dhidi ya Polisi Tanzania ikishinda mabao 2-1 na Coastal Union ilipoondoka na mabao 2-0 dhidi ya wenyeji, mpaka sasa ikishika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi sita sawa na Simba iliyoko kileleni kutokana na kushinda 3-0 dhidi ya Geita Gold FC na 2-0 dhidi ya Kagera Sugar.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >